# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 9 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tisa, Kikao cha Ishirini na Moja, leo tarehe 9 Mei, 2025.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali yetu kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Busokelo aulize swali lake.

Na. 262

**Kukamilisha Ujenzi wa Vituo vya Afya - Busokelo**

**MHE. ORAN M. NJEZA K.n.y. MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya Mpata, Isange na Ntaba – Busokelo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vya Mpata, Isange na Ntaba jumla ya shilingi milioni 491 zinahitajika. Kituo cha Afya Mpata kinahitaji shilingi milioni 395, Kituo cha Afya Isange shilingi milioni 76 na Kituo cha Afya Ntaba shilingi milioni 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetoa shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vya Mpata, Isange na Ntaba katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi viporo ya vituo vya afya nchini ikiwa ni pamoja na Vituo vya Afya vya Mpata, Isange na Ntaba, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali.

Kwa kuwa Serikali imetenga na mahitaji makubwa kwa vituo hivyo ni majengo ya *OPD* pamoja na upasuaji. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo hayo?

Swali la pili, kwa kuwa wananchi wa Kata za Ilungu, Iwindi pamoja na Kata ya Ulenje wameshajenga vituo vya afya kwa hatua kubwa. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo hayo ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nianze kwa kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Busokelo kwa namna ambavyo wamekuwa wakishiriki katika kuchangia nguvu zao katika ujenzi wa vituo vya afya na Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kutenga fedha na kuwapelekea fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi vya afya, lakini tunafahamu kwamba ujenzi wa vituo hivi unakwenda kwa awamu. Serikali imeshapeleka fedha katika vituo hivi vitatu na tunafahamu kuna majengo ambayo bado yanahitajika, yakiwepo majengo ya *OPD* na jengo la upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Busekelo kwamba Serikali inafahamu na imeshaingiza kwenye mpango wa vituo vinavyohitaji fedha kwa ajili ya umaliziaji na tutahakikisha tunapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha vituo hivi vya afya ikiwemo ujenzi wa majengo ya *OPD*, jengo la upasuaji na majengo mengine ambayo yanapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili niwapongeze wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini ma Mheshimiwa Mbunge, kwa namna ambavyo wamejenga vituo hivyo vya afya, lakini nimhakikishie tu kwamba tayari Serikali ilishaweka utaratibu madhubuti wa kutambua vituo vya afya vyote ambavyo vimejengwa kwa nguvu za wananchi, lakini zahanati na kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kukamilisha vituo hivyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Oran Njeza, nikuhakikishie tu kwamba tunafahamu na tunatenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa vituo hivyo vya afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuendelea kufanya kazi kubwa ya kuendelea kuweka fedha kwa ajili ya miundombinu ya afya.

Je, ni lini Serikali itakamilisha miundombinu katika vituo vya afya; Kituo cha Afya Endasak, Nangwa, Gisambalang pamoja na Masqaroda Jimbo la Hanang? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwanza ilishatambua kata za kimkakati katika Jimbo la Hanang na ilikwisha peleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, lakini tunafahamu kwamba vipo vituo vya afya ambavyo havijakamilika kama ambavyo Mheshimiwa Asia Halamga amesema; Kituo cha Afya cha Nangwa, Gisambalang, Endasak na Masqaroda. Nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari vimeshaingizwa kwenye mpango kwa ajili ya kuingizwa kwenye bajeti kwa awamu, kwa ajili ya kukamilisha vituo hivyo ili vitoe huduma bora zaidi kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylvia.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Tanzania aliahidi shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kasanga Wilaya ya Kalambo, shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo pamoja na gari la wagonjwa, lakini tangu mwaka 2020 mpaka leo hatujapata fedha hizo. Je, nini kauli ya Serikali katika kutimiza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Serikali kwa ujumla moja ya vipaumbele ambavyo vinawekwa kwenye mipango ya utekelezaji ni ahadi na maelekezo ya viongozi wa kitaifa na tunafahamu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kituo cha afya na tayari tumeshakiingiza kwenye mpango wa Benki ya Dunia na wakati wowote kituo hiko cha afya kitajengwa katika halmashauri ya Kalambo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Butondo, nilikuona.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, wananchi wa Kata ya Sekebugolo wameanzisha Kituo cha Afya cha Dulisi ambapo *OPD* ndio imekuwa ikitumika, wameanza kwa hatua ya awali. Je, Serikali ni lini itafanya ukamilishaji wa kituo kile ili kiwe na hadhi maalumu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Jimbo la Kishapu kwa Mheshimiwa Butondo ni moja ya majimbo ambayo Serikali imeendelea kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, lakini Serikali pia ilishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri

kutenga fedha za mapato ya ndani kwa kushirikiana na nguvu za wananchi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo na Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha vituo hivyo, wataalamu na vifaatiba pamoja na madawa.

Naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Buntondo kwamba tunafahamu na tayari tumeingiza kwenye mpango na tutatafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha kituo hicho cha afya ili tuweze kutoa huduma bora kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha afya Rutunguru na Kituo cha Afya Mabila ni lini Serikali itapeleka fedha ili kiweze kutumika kwa huduma zote? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi na ukamilishaji wa vituo vya afya unafanyika kwa awamu na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Jimbo la Kyerwa litapelekewa fedha kwa awamu kwa ajili ya kukamilisha vituo hivyo vya afya, lakini pia maboma ya zahanati kwa kadiri ambavyo ameyawasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza niishukuru Serikali kwa kuendelea kujenga vituo vya afya maeneo mbalimbali. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Mwasai, Wilaya ya Maswa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nishatembelea kata ile ya Mwasai na niliona kazi nzuri ya ujenzi ambayo Serikali ishapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo kile cha Afya cha Mwasai katika Halmashauri ya Maswa na nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hilo ni endelevu, tutaendelea kutenga fedha kwa awamu na kukamilisha miundombinu yote ambayo inabaki ili tuhakikishe kituo kile kinakuwa na majengo yote muhimu kwa ajili ya huduma hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, nilikuona.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilituahidi kutujengea vituo vitatu vya kimkakati na katika vile tulipata kimoja kile cha Mareu, tunasema ahsante kwa ajili ya hicho kituo, lakini sasa kuna hivi vituo vingine viwili vilivyobaki sijui vilienda wapi Mheshimiwa Waziri? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita na Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kusogeza sana huduma za afya karibu na wananchi kwa kutambua kata zote za kimkakati na kupeleka fedha na hivi karibuni Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi tulikuwa na ahadi ya muda mrefu ya Serikali ya kuleta vituo vya afya kwa kila jimbo, tumeanza na majimbo 120 na nafahamu jimbo la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo pia limo.

Kwa hiyo, katika vituo hivyo vya afya vitatu tayari kimoja kimeshapelekewa fedha, kimoja kitapelekewa fedha hivi karibuni lakini na hicho kingine ni kuhakikishie Mheshimiwa Dkt. Pallangyo

na wananchi wa Jimbo la Arumeru kwamba fedha hiyo itapelekwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vituo hivyo vya afya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara.

Na. 263

**Maafisa Ugani Kupewa Mafuta Ili Kutoa Huduma kwa Wananchi**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kuwawezesha Maafisa Ugani kwa kuwapa mafuta ili waweze kutembelea wakulima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua majukumu muhimu yanayofanywa na Maafisa Ugani katika kutekeleza majukumu yao kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ili kuwawezesha Maafisa Ugani kutekeleza majukumu yao katika halmashauri, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo mpaka kufikia Machi, 2025 imewapatia wataalamu hao vitendea kazi mbalimbali zikiwemo pikipiki 6,444, vishikwambi 5,426, sare 6,456 na magari 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya mikoa mitano, halmashauri 12 zimetenga bajeti ya mafuta kati ya lita 10 hadi 15 kwa kila mwezi kwa ajili ya kuwawezesha Maafisa Ugani kutekeleza majukumu yao. Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri zitaendelea kutenga bajeti ya fedha kwa ajili ya mafuta na matengenezo ya pikipiki za Maafisa Ugani ili waweze kutekeleza majukumu yao na kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri husika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, ambapo kwa kweli tunaona Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeupiga mwingi kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka wa kutenga mfuko maalumu kwa ajili ya maafisa ugani nchini, ili uweze kutumika kuwawezesha kupata mafuta na posho nyingine wanazozihitaji wakiwemo Maafisa Ugani wa Ngara ili waendeleze kazi nzuri ambayo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu hasa kazi ya kilimo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali inatambua sana kazi nzuri na kubwa inayofanywa na Maafisa Ugani katika kutoa elimu, kusimamia shughuli za Kilimo na kukutana na wananchi mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba tunaboresha shughuli za kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba wazo alilolitoa la kuwa na mfuko maalumu kwa ajili ya Maafisa Ugani, sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Serikali kwa ujumla tumelichukua kama pendekezo, tutalifanyia tathmini na kuona kama linatekelezeka kwa utaratibu gani na kama kuna maboresho mengine mbadala basi Serikali itaendelea kufanya hivyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge wa Ilemela, kwa niaba Mheshimiwa Shally Raymond.

Na. 264

**Ujenzi wa Uzio Katika Shule za Msingi Nchini**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga uzio katika Shule za msingi ambazo hazina uzio maeneo ya mijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya elimu nchini ikiwa ni pamoja na kujenga uzio katika shule mbalimbali za msingi kwa kuzipa kipaumbele shule zenye watoto wenye mahitaji maalumu. Katika mwaka 2022/2023 na 2023/2024 Serikali imetoa shilingi bilioni 5.57 kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika shule 185 za watoto wenye mahitaji maalumu. Vilevile, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikitenga fedha kupitia mapato ya ndani kujenga uzio ili kuimarisha ulinzi katika maeneo yenye changamoto za kiusalama. Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri itaendelea kutenga fedha za ujenzi wa uzio kwa ajili ya usalama wa wanafunzi na mali za shule kadiri ya upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri sana kutoa hela hizo, lakini je, Jimbo la Ilemela limefanikiwa katika fungu hilo?

Swali la pili, kwa kuwa shule nyingi za *primary* zipo barabarani, zikiwemo hata zile za vijijini na kule Kata ya Uru Kusini Shule ya Okaseni ipo barabarani kabisa, mpira ukiteleza tu gari linapita watoto wanapata ajali. Ni lini sasa itakuwa ni azimio

muhimu kwamba shule zote za *primary* za mjini na vijijini zijengewe uzio? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Jimbo la Ilemela ni moja ya majimbo ambayo yamenufaika kwa fedha ambazo zimepelekwa kwa ajili ya ujenzi wa uzio, zikiwemo hizi shilingi bilioni 5.57 ambazo Serikali imezitoa, lakini nitumie nafasi hii kuendelea kuwasisitiza wakurugenzi wa Mamlaka Serikali za Mitaa kwamba ni wajibu wao na wanawajibika kuhakikisha wanatambua shule zote ambazo zina mazingira hatarishi na kutenga fedha za mapato ya ndani kwa awamu kwa ajili ya kujenga uzio ili kuhakikisha watoto wetu wanakuwa salama zaidi na Serikali Kuu itaendelea kutoa fedha hizo kwa awamu ili kuhakikisha watoto wetu wanakuwa salama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kweli zipo shule ambazo zipo kandokando ya barabara kuu na ni hatarishi zaidi kwa wanafunzi na Serikali ina mpango huo na imeanza kuutekeleza mpango wa kuzitambua shule ambazo zina mazingira hatarishi kwa maana ya *geographical location,* lakini pia kwa shule zile ambazo zina watoto wenye mahitaji maalumu na imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa uzio.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa mama yangu, Mama Shally Raymond kwamba tutaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha watoto wetu wapo katika mazingira salama zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya mabadiliko makubwa ndani ya muda

mfupi kuhakikisha inaendelea kumuinua mtoto wa kike katika elimu, ikiwemo kuwarudisha mabinti waliyokuwa wamepata ujauzito shuleni, lakini pia ujenzi wa shule 26 za wasichana katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Sasa baadhi ya shule hizi bado hazina uzio, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha shule hizi zinawekewa uzio ili kuendeleza ulinzi wa mtoto wa kike pale anapokuwa anapata elimu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya mapinduzi makubwa katika sekta ya elimu kwa ujumla, lakini pia katika eneo la elimu ya mtoto wa kike kwa kujenga shule kubwa za sayansi za kila mkoa, shule 26 ambazo zote zimekamilika na watoto wetu wameanza kupata masomo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Ng'wasi Kamani, kwamba Serikali ilishaweka bajeti na ishaandaa *master plan* kwa ajili ya kujenga uzio kwenye shule zote za sekondari za mikoa ili kuhakikisha kwamba watoto wetu wanakuwa katika mazingira salama zaidi, lakini pia na shule nyingine ambazo zipo katika maeneo hatarishi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, nilikuona.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, kwa kuwa shule za sekondari na za msingi Moshi Mjini kupitia ma-*group* ya *alumni* pamoja na wananchi na wazazi wameanza kujenga ukuta na kwa kuwa na mimi pia nimeunga juhudi hizo kwa kuwapa shilingi milioni 4.5 shule nne; Shule ya Sekondari ya JK, Shule ya Sekondari ya Karanga, Shule ya Msingi Kiusa na Shule ya Sekondari Kiusa kila moja shilingi milioni 4.5 kuunga mkono juhudi hizo. Je, Serikali ipo tayari sasa kuwasaidia wakamilishe kuweka uzio katika shule hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza, nimpongeze sana Mbunge wa Moshi Mjini, Mheshimiwa Tarimo kwa kutoa kiasi hicho cha shilingi milioni 4.5 kuunga mkono juhudi za wananchi, wazazi na *alumni* ambao wanachangia kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika shule hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie tu pamoja na jitihada hizo za wananchi, Mbunge pamoja na wadau Serikali pia imeendelea kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika maeneo hayo na nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Jimbo la Moshi Mjini kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu ili kuunga mkono juhudi hizo na kuhakikisha kwamba shule hizo zinajengewa uzio. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, nilikuona.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, pamoja na tatizo hilo la uzio katika shule za mijini, zipo shule za vijijini pia ambazo zinakosa uzio na zipo hatarini kuingiliwa na wanyama wakali pamoja na mifugo kama ng'ombe. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba shule za vijiji na zenyewe zinawekewa uzio? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali iliweka mpango wa kujenga uzio katika shule zetu zote kwa awamu, lakini kwa kipaumbele ni zile shule zenye mazingira hatarishi zaidi bila kujali ni shule za mijini au vijijini ilimradi mazingira yake ni hatarishi zaidi basi Serikali imeendelea kuweka kipaumbele zaidi kwa ajili ya ujenzi wa uzio.

Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata shule za vijijini ambazo zina mazingira hatarishi zaidi zimepewa kipaumbele na zipo shule ambazo tayari zimejengewa uzio na zoezi hili ni endelevu Serikali itaendelea kuteka fedha kwa

ajili ya kujenga uzio katika shule hizo ili kuhakikisha usalama kwa wanafunzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

Na. 265

**Ukarabati Barabara za Mitaa Nchini**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha barabara za mitaani zinafanyiwa ukarabati na maboresho ili kuepusha usumbufu wakati wa mvua?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Serikali iliongeza bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni 275 hadi shilingi bilioni 870.3 ongezeko la shilingi bilioni 595.3, sawa na 216%, lengo likiwa ni kuijengea uwezo *TARURA* kuzihudumia barabara zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali hutenga fedha ya dharura shilingi bilioni 21 katika bajeti kila mwaka ili kukabiliana na athari zinazosababishwa na mvua. Katika mwaka 2023/2024 Serikali ilitoa shilingi bilioni 84.36 kutokana na mvua za *El Nino* zilizoleta madhara makubwa katika barabara hapa nchini na katika mwaka wa fedha 2024/2025 imetoa shilingi bilioni 11.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuujengea uwezo wa kibajeti wa *TARURA* kulingana na upatikanaji wa fedha

ili uweze kuzikarabati barabara za mitaa na kuwa tayari hasa nyakati mvua za masika na vuli zinaponyesha, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninaomba niulize maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mtandika - Ikula kilometa 18 katika Kata ya Ruaha Mbuyuni hii barabara haipitiki. Ni lini sasa itakarabatiwa ili iweze kupitika hata pikipiki ziweze kupita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Ndengisivili - Kimala pia ipo katika Kata ya Kimala ni lini itakarabatiwa? Kwa sababu kuna maeneo tu machache ambayo yamekuwa korofi hayapitiki wakati wote wa mvua. Je, lini sasa Serikali itaangalia maeneo ambayo korofi yaweze kukarabatiwa ili barabara ziweze kupitika kwa mwaka mzima? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli zipo baadhi ya barabara ambazo zimeathirika na mvua na mafuriko, lakini pia zipo barabara ambazo hazijafanyiwa matengenezo ya mara kwa mara kwa muda mrefu na Serikali imekwishazitambua barabara hizo zote zikiwemo barabara za Wilaya ya Kilolo barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja Mtandika - Ikula ya kilometa 18 na Ndengisivili - Kimala ambazo hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza nimkumbushe na kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa Iringa na wa Wilaya ya Kilolo kuhakikisha kwamba wanazifanyia tathmini haraka barabara hizi na kujua gharama inayohitajika ili waweze kuleta maombi hayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya ukarabati ili angalau ziweze kupitika vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Tima - Mapemba - Oysterbay hadi Kwa Mapunda umeshasainiwa. Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo kulingana na mkataba utaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya taratibu baada ya kusaini mikataba kuna taratibu ambazo wakandarasi wanafanya zikiwemo *mobilization,* lakini pia mara nyingine *advance payment*. Kwa hiyo, nikuhakikishie tu barabara hii ambayo umeitaja Mbunge wa Mbagala, Mheshimiwa Chaurembo, tumesaini maktaba kama ulivyosema hatua zinazofuata sisi Serikali tutaisukuma kwa haraka zaidi ili mkandarasi aanze ujenzi mapema iwezekanavyo ili wananchi waweze kunufaika na mpango huo mzuri wa Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi, Barabara ya Liwale - Nahoro, Liwale – Mpigamiti, Liwale – Ndapata, Liwale - Kikulyungu ni barabara zilizoharibika sana na mvua hizi zinazoendelea. Nini mpango wa Serikali kuzifanyia ukarabati barabara hizi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya Majimbo ambayo yamepata kipaumbele cha bajeti ya fedha za *TARURA* ni pamoja na Jimbo la Liwale

kutokana na kuathirika kwa kiasi kikubwa na mvua, lakini barabara zake nyingi zilikuwa zimeharibika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hizo tunazitambua na tumeziweka kwenye mpango kwa ajili ya ukarabati kwa awamu. Niwahakikishie wananchi wa Jimbo la Liwale kwamba Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, itaendelea kupeleka fedha kwa awamu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara hizo zinapitika vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasalali na Mheshimiwa Saashisha, nimewaona.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, mwaka 2022/2023 Serikali ilipeleka pesa kwa ajili ya kujenga Barabara ya kutokea Ilumba – Mwakaluto - Goloma ambayo ilikuwa ni muhimu sana kwa ajili ya kupitisha mazao, lakini barabara hii kwa sasa kutokana na mvua imesombwa yote haipitiki.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kupeleka pesa ya dharura ili barabara hii muhimu kwa Jimbo ya Sumve iweze kujengwa upya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaona umuhimu wa kupeleka fedha kwenye barabara hiyo katika Jimbo la Sumve, Wilaya ya Kwimba na nitumie nafasi kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, TAMISEMI kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Wilaya Kwimba na Mkoa wa Mwanza kuifanyia tathmini barabara hiyo, kujua gharama zinazohitajika kwa ajili ya matengenezo maeneo korofi ili Ofisi ya Rais, TAMISEMI iweze kupeleka fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara hizo zinafanyiwa matengenezo na zinaanza kupitika vizuri zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Saashisha, Mheshimiwa Aziza nimekuona.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mvua zinazoendelea kunyesha katika Jimbo la Hai zimefanya uharibifu mkubwa wa barabara; Barabara ya Mferejini - Kwa Tito – Boma - Kikavu Chini pale Kisereni, Kwa Mengi kwenda Kiria - Somali kwenda Tindigani, Tindigani kwenda Rundugai lakini pia Barabara ya Makoa Mferejini eneo la Kwa Mengi pale na barabara nyingine nyingi hazipitiki kwa sasa.

Je, Serikali ina mpango wa haraka wa kufanya ukarabati barabara hizi ili ziweze kupitika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mvua ambazo zimeendelea kunyesha kote nchini zimekuwa na madhara mbalimbali kwenye barabara zikiwemo barabara za Jimbo la Hai na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hizo zote ambazo amezitaja kwa bahati nzuri ameshazileta kwa maandishi Ofisi ya Rais, TAMISEMI na sisi tumeshaweka kwenye mpango kwa awamu kwa ajili ya kuzikarabati ziweze kupitika.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Hai kwamba Serikali itazifanyia kazi barabara hizo ili ziweze kupitika vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara. Nilimwita Mheshimiwa Aziza kwanza, halafu baadaye Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Kwa kuwa barabara hizi zinasimamiwa na *TARURA*. Serikali imeongezea kiwango kikubwa cha pesa *TARURA,* lakini bado barabara zina shida za kuweza kupitika. Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia Mfuko huu wa *TARURA* ili barabara hizi ziweze

kupitika kwa muda mrefu zaidi kuliko sasa pesa zinakwenda, lakini bado barabara zinakuwa mbovu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme jambo moja muhimu kwamba katika kipindi hiki cha miaka minne Serikali imeongeza sana mtandao wa barabara za *TARURA*. Kwa hiyo, barabara nyingi mpya zimeendelea kufunguliwa na kujengwa na hiyo imepelekea mahitaji ya fedha za barabara kuendelea kuongezeka na Serikali imeongeza bajeti ya barabara kutoka shilingi bilioni 275 mwaka wa fedha 2021/2022 mpaka shilingi bilioni 870.3 mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ambayo Bunge hili Tukufu imepitisha wiki mbili zilizopita Mheshimiwa Rais ameongeza tena bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni 870.3 mpaka shilingi trilioni 1.130. Kwa hiyo, jitihada za Serikali zipo wazi za kuongeza fedha na uwezo wa *TARURA* na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba barabara hizo zinazoathirika zitaendelea kujengwa kwa awamu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara, halafu nimemuona Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, kwanza, ninaishukuru sana Serikali kupeleka fedha shilingi milioni 400 kujenga Daraja la Mto Tigite kuunganisha pale Matongo. Kuna ahadi ya Mawaziri wa TAMISEMI wawili waliopita kutoa kilometa moja ya lami Sirari - Nyamongo na Halmashauri ya Nyamwaga Makao Makuu.

Je, ni lini ahadi hiyo ya Serikali itatekelezwa katika maeneo yale pale, ukizingatia kwamba Tarime ni Jimbo la Kanda Maalum na mambo yake ni maalumu sana? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni kwamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alifanya ziara katika Jimbo la Tarime Vijijini na akatoa ahadi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kilometa moja katika eneo hilo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja. Ninaomba nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Jimbo la Tarime Vijijini kwamba Serikali ikiahidi inatekeleza na sisi sote ni mashahidi kwamba ahadi zote ambazo Serikali imekuwa ikitoa imekuwa ikitekeleza. Kwa hiyo, wananchi wawe na amani, Serikali ipo kwenye hatua nzuri za kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza kujenga barabara hiyo kwa awamu ili iweze kuwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Maimuna Mtanda, atamalizia Mheshimiwa Minza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi; ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya barabara ambazo zipo Jimbo la Newala Vijijini zisizopitika hasa Mkoma II kwenda Chimemena lakini pia ile ya Malatu Shuleni - Mchauru hadi Mpalu ili ziweze kupitika kwa urahisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaje hiyo ya Mkoma II kwenda Chimemena na nyingine zote ni moja ya barabara ambazo Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* inazitambua, imeziainisha na inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kuzitengeneza ili ziweze kupitika vizuri.

Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mtanda na Wananchi wa Jimbo la Newala Vijijini kwa Serikali tayari imezitambua na tayari inatenga bajeti kwa awamu na barabara hizo zitatengenezwa ili ziweze kupitika vizuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza, nilikutaja.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi za Mkoa wa Simiyu zile za ndani zote zimekatika na wakulima wanapata shida sana kusafirisha mazao kutoka shambani kupeleka nyumbani, vivyo hivyo na wafanyabiashara ni tatizo kubwa. Je, ni lini Serikali itakarabati barabara hizo ili wananchi wa Mkoa wa Simiyu wafanye kazi kwa ufanisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mikoa ambayo imepata kipaumbele kikubwa cha fedha za barabara kwa ajili ya ukarabati barabara za vijijini na mijini ni Mkoa wa Simiyu na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa tunapoongea Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini katika Mkoa wa Simiyu wanaendelea na ukarabati wa barabara makalvati na madaraja katika maeneo mbalimbali na hizo barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja nimhakikishie tu kwamba Serikali itazifikia kwa ajili ya kuzikarabati na kuhakikisha kwamba zinapitika vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi; Mji wa Bunda unakua, lakini cha ajabu barabara ya lami ipo moja tu kutoka pale kwenda Bomani na Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya alituahidi kutujengea barabara ya lami kilometa moja, moja katika Mitaa ya Bunda. Ni lini sasa mtatujengea barabara ya lami kwenye Mitaa ya Bunda ili iendane na hadhi ya Mji wa Bunda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mji wa Bunda unakuwa kwa kasi na Mheshimiwa Mbunge mara kwa mara amekuwa akiwasemea pia wananchi wa eneo la Bunda kwa ajili ya kuona miundombinu inakuwa vizuri na mimi ninaomba nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini, kwamba Serikali inatambua uhitaji wa barabara za lami na ahadi za viongozi wetu wa kitaifa ni kipaumbele na tutakwenda kutekeleza ujenzi wa barabara hizo kwa awamu.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Ester Bulaya na Wananchi wa Bunda Mjini kwamba Serikali hii sikivu itakwenda kujenga barabara hizo kwa awamu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo yote ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 266

**Kukamilika kwa Mradi wa Halmashauri Bonde la Rukwa**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** Aliuliza: -

Je, lini Mradi wa Umwagiliaji Bonde la Rukwa wenye thamani ya shilingi bilioni 21 utakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ujenzi wa Skimu ya Ilemba wenye thamani ya shilingi bilioni 21 ulitarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2024. Hata hivyo, ujenzi huo haukukamilika

kutokana na mvua za *El-Nino* za mwaka 2023/2024 pamoja na mvua nyingi za masika zinazoendelea mkoani Rukwa kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefanya tathmini ya muda uliopotea kutokana na mvua nyingi zilizosababisha kusimama kwa kazi na kuongeza muda wa utekelezaji wa mradi hadi mwezi Disemba, 2025. Ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa muda uliopangwa, Tume itaendelea kumsimamia mkandarasi husika kwa karibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza haya maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kabisa niipongeze sana Serikali kwa kututengea fedha nyingi sana shilingi bilioni 21 siyo kitu kidogo, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua sasa Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika kwa wakati, kwa sababu wananchi walikuwa wana mategemeo makubwa sana kutokana na ukame uliojitokeza. Kwa hiyo, walikuwa na mategemeo makubwa sana na mradi huu. Ni lini sasa Serikali itahakikisha mradi huu unakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Wilaya ya Nkasi, Jimbo la Nkasi Kusini halijapata mradi wa umwagiliaji hata mmoja. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha na jimbo hilo linapata mradi mmoja wa umwagiliaji? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata kwa kazi nzuri ya kufuatilia miradi katika Mkoa wake wa Rukwa hususani ya kilimo. Jambo moja tu nimthibitishie kwamba huu mradi utakamilika kama tulivyopanga inapofika Disemba mwaka huu, kwa sababu fedha tumeshampatia mkandarasi na tumeshawaelekeza watu wa Tume katika Kanda

ile ya mkoa wenu kuhakikisha wanafuatilia kwa karibu ili wale wananchi wa kule bondeni waweze kufaidika na huu mradi. Kwa hiyo, tutaendelea kufuatilia kwa karibu kuhakikisha unakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kulipatia mradi Jimbo la Nkasi Kusini kwa ndugu yangu Mheshimiwa Mbogo, nikushukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kwamba hili jambo lipo na tunafanya tathmini katika yale maeneo ambayo yanafaa. Tukishamaliza ile tathmini maana yake tutajenga miradi kama ambavyo wewe umetoa maelezo na Mbunge alishatuletea maombi katika eneo hilo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, kwa kuwa mkandarasi atakayejenga Mradi wa Arusha Chini uliopo Kata ya Chawi na Kiromba ameshapatikana. Je, ni lini utekelezaji wa mradi huu utaanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni kwamba ninatambua mradi huu kwenye Jimbo la Mheshimiwa Chikota, upo katika hatua ya mkandarasi kufanya *mobilization* kupeleka vifaa kwa sababu tayari tumeshamlipa *advance payment*. Kwa hiyo, nimthibitishie tu kwamba tutamharakisha mkandarasi ili anze kazi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, nilikuona.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutembelea Jimbo la Vunjo na kujionea kero nyingi kwenye masoko yetu, lakini pia kuona lile Bwawa la Urenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kama bwawa hili ambalo lina uwezo mkubwa wa kuwezesha kilimo cha uwangiliaji kwenye Kata ya Kirua Vunjo

Mashariki kama hili bwawa limeingizwa sasa kwenye bajeti ya mwaka huu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umemwelewa Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewelewa.

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni kwamba ni kweli nilipita Vunjo kwa Mheshimiwa Dkt. Kimei na tulitembelea hilo Bwawa la Kweka na tuliona kabisa umuhimu na tuliwaelekeza watu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mkoa wake kufanya tathmini na wameshafanya tathmini wameshatuletea. Tunachofanya sasa hivi ni kutafuta fedha ili tathmini hiyo ifanyike ili sasa tuweze kwenda kuliongeza upana na wale wananchi waweze kufaidika na mradi ule wa eneo la Kirua Vunjo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso, nilikuona.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, *Scheme* ya Karema ni ya muda mrefu na Serikali iliahidi kutoa fedha kwa ajili ya kuikamilisha hiyo *scheme*, ni lini Serikali itapeleka fedha walizoahidi shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kukamilisha *scheme* hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni kweli tunatambua umuhimu wa *Scheme* ya Karema na hatua ambayo tunamalizia ni kufanya tathmini ili sasa tupeleke fedha kwa sababu *scheme* ile ni kubwa sana na itakuwa na faida kubwa kwa wananchi wa jimbo lake. Kwa hiyo, nimwondoe tu shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba hili tunalitambua na tumelipa umuhimu mkubwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Monni, nilikuona.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, mwaka 2024/2025 tulipitisha bajeti hapa na zikatengwa fedha kwa ajili ya Bwawa la Ndoroboni na Babayo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, ninaomba kujua ninaona bajeti inaishia kikomo mwezi wa sita na mpaka leo ujenzi haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujua ni lini watatoa fedha ili kuanza ujenzi wa mabwawa hayo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni kweli anachokisema Mbunge wa Jimbo la Chemba Mheshimiwa Monni. Haya mabwawa tulishayaweka katika bajeti yetu na kiukweli tulishatangaza kupata kwa ajili ya ukandarasi na tumeshaomba fedha Wizara ya Fedha na wametuahidi kutupatia na kwa sababu mwaka wa fedha bado mpaka mwisho wa mwezi wa sita, tutapeleka fedha ili miradi hii ianze kutekelezwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mradi wa Umwagiliaji Kata ya Litumbandiosi kwa muda mrefu upo kwenye upembuzi yakinifu, ni lini sasa utaanza kujengwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimthibitishie tu Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini, Mheshimiwa Benaya kwamba mradi huu sisi tumeshamaliza tathmini ya mwisho na sasa hivi tupo katika hatua ya kumtafuta mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kwa hiyo, wathibitishie tu wananchi wako kwamba mradi ule utajengwa na jitihada zile kubwa na wewe ni sehemu ya watu ambao wameifanya, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Salim Mussa Omar, Mbunge wa Gando, litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

Na. 267

**_NFRA_ Kujitegemea**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI K.n.y. MHE. SALIM MUSSA OMAR** Aliuliza: -

Je, ni upi mpango wa Serikali kuifanya *NFRA* kujitegemea hususan Idara ya Vyakula ili kuepuka uhaba wa chakula pindi nchi tegemezi zinapokumbwa na majanga?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** Alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha uwezo wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* ili ijitegemee na kupunguza utegemezi wa Serikali bila kuathiri jukumu lake la msingi la kuhakikisha usalama wa chakula nchini, Serikali ina mikakati ifuatayo:-

(i) Kuongeza uwezo wa kuhifadhi chakula kutoka tani 776,000 wa sasa hadi tani 3,000,000 ifikapo mwaka 2030. Hatua hiyo itafikiwa kwa kukarabati na kujenga vihenge na maghala ya kisasa na hivyo kuwezesha kudhibiti upotevu wa mazao baada ya mavuno;

(ii) Kuimarisha mifumo ya ununuzi na usambazaji ikiwemo matumizi ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha upatikanaji wa chakula kwa haraka katika maeneo yenye changamoto; na

(iii) Kuimarisha uwezo wa kibajeti kwa kuongeza vyanzo vya mapato ikiwemo uzinduzi wa Hati Fungani ya Usalama wa Chakula *(Food Security Bond)*. Hati hii inalenga kuongeza

mtaji kwa ajili ya uboreshaji zaidi wa miundombinu, upanuzi wa shughuli za kibiashara na utekelezaji wa mikakati ya muda mrefu ya usalama wa chakula nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pamoja na majibu mazuri ninaomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NFRA* wamekuwa wakikopa pesa kwenye taasisi za kibenki na kimsingi tunapokopa pesa kwenye taasisi za kibenki kumekuwa na riba jambo ambalo limekuwa likiirudisha nyuma *NFRA* katika utekelezaji wake mahsusi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia pesa *NFRA* ili iweze kujitegemea na kuachana na suala la ukopaji kwa sababu linawarudisha nyuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali (b), kukodi maghala imekuwa ni jambo ambalo kwanza maghala yanakodiwa mengi, lakini pia ni pesa nyingi sana ambayo *NFRA* imekuwa ikitumia na mpango huu ni wa muda mrefu sasa, *NFRA* bado haijaanza kujenga.

Je, ni lini Serikali itaenda kujenga maghala kwa haraka katika maeneo ya Kigonsera, Liganga, Namtumbo pamoja na Mgazini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nimpongeze sana muuliza maswali ya nyongeza dada yangu Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Ruvuma na hii imekuwa ni moja ya ajenda yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja awe na uhakika nalo kwamba moja *NFRA* Serikali kupitia bajeti tumekuwa tukitenga

fedha kila mwaka kwa ajili ya kununua chakula, hilo ni moja na la uhakika na la kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kukopa ni sehemu ya *NFRA* kujijengea uwezo wa kujiendesha kibiashara kwa sababu wakikopa bahati nzuri huwa wanarudisha zile fedha kwa sababu tumekuwa tukifanya biashara na nchi jirani za yale mazao ambayo tumekuwa tukiyanunua hapa nchini. Lakini Serikali haitaacha jitihada zake za kuongeza fedha ili kuhakikisha kwamba *NFRA* inapata uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba sasa tunakwenda kuwa na hati fungani ya usalama wa chakula ambayo sasa itaongeza mtaji mkubwa na kupunguza *NFRA* kwenda kukopa katika taasisi za kifedha. Kwa hiyo, hilo nimthibitishie tu tupo katika mpango kabambe kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujenga maghala, huo ni mpango wa Serikali na mpango tulionao ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na maghala ya chakula katika halmashauri zote nchini na ndiyo maana unasema tunataka kutoka tani 700,000 za sasa kwenda tani milioni tatu. Sasa ili uweze kufikia ni lazima tupeleke maeneo yote ili hata kwenye yale maeneo wakati mwingine yakifikiwa na njaa iwe rahisi wale wananchi kukipata chakula katika maeneo ya karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ndiyo mipango ya Serikali ambayo tupo nayo sasa hivi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Kilimo.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa aulize swali lake.

Na. 268

**Ujenzi wa Barabara ya Mkiu – Liganga – Madaba (Km 112)**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** Aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa barabara ya Mkiu – Liganga – Madaba utaanza kwa kiwango cha lami kwa kuwa uwekezaji wa Liganga upo mbioni kuanza?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** Alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Mkiu – Liganga – Madaba yenye urefu wa kilometa 112 imekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali na ningependa kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali bado inatafuta fedha kwa ajili ya hii Barabara ya Mkiu – Liganga – Madaba na ile inayopita Liganga inayouganisha Mchuchuma kupitia Ibumi, je, Serikali haioni haja ya kuongeza fedha kwa ajili ya matengenezo ya kawaida hasa maeneo yale ya Ligangalanzuki pale Shaurimoyo na kule Ndolela upande wa Madaba ili shughuli za wananchi zisiathirike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, barabara ile ya Itoni – Ludewa – Manda, sehemu ya Itoni - Lusitu imesimama kwa muda mrefu, mimi na Mheshimiwa Mwanyika tumekuwa tukiisemea sana na sasa Chama cha Wasafirishaji Abiria Mkoa wa Njombe wameandika barua kwamba wana kusudio la kusitisha usafiri wa

wananchi maeneo yale. Je, ni lini barabara hii itaweza kuendelea kutengenezwa na je, Serikali ipo tayari kukutana na hawa Chama cha Wasafirishaji Abiria Mkoa wa Njombe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsnate, ninaomba kujibu maswlai mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hii barabara aliyosema ni moja ya barabara ya kimkakati kwa maana ya nchi kwa sababu ndiyo inayoenda ambapo kuna uwekezaji mkubwa sana wa chuma na wakati Serikali inatafuta chanzo cha uhakika cha fedha ili tuweze kuijenga hii barabara ambayo sehemu hii tunajenga kwa utaratibu wa zege kwa sababu ya ukubwa wa mzigo utakaotoka huko, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumetenga fedha za kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika na tambua kwamba sasa hivi mvua zinanyesha nyingi sana, lakini tulishawaelekeza mameneja, na labda nitumie nafasi hii kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa katika kipindi hiki hasa cha mvua wanaendelea kufanya matengenezo ili kufanya barabara hizi zipitike japo katika kipindi hiki cha mvua huwa hatuwekezi fedha nyingi sana kwa sababu hasa kwenye hizi barabara ambazo sio za lami kwa sababu unaweza ukawekeza halafu ikaondoka, tunafanya tu ili barabara hizi ziweze kupitika. Kwa hiyo, meneja alishaelekezwa afanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Itoni - Lusitu, mkandarasi yupo *site* tumeshamlipa sehemu ya malipo ya fedha alizokuwa anadai na tuna uhakika kwamba muda sio mrefu tutakamilisha yale malipo yote ili aendelee kufanya kazi na tumeshampa maelekezo huyo meneja mahali ambako kuna *diversion* ahakikishe kwamba barabara hii inapitika muda wote, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus nilikuona na Mheshimiwa Erick, maswali ninaomba yawe mafupi.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa usanifu wa Barabara ya Mwanza – Busisi ulishakamilika, *tender* ilishatangazwa na *traffic* ni kubwa sana, magari zaidi ya 15,000 kwa siku. Mheshimiwa Waziri ni lini Barabara ya Mwanza – Usagara mkandarasi atatangazwa na kuanza utekelezaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha bajeti na hata katika bajeti kujenga hii barabara kwa njia nne Mwanza ilitamkwa na ipo na ni mpango pia wa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tulishampata mkandarasi ambacho tunafanya sasa hivi ni majadiliano *(negotiation)* ili tuweze kufikia kwenye maeneo ambayo tutakubaliana kwenye upande wa Serikali na yeye ili hatimaye sasa aanze kuijenga hiyo barabara. Kwa hiyo, ni kipaumbele kikubwa cha Serikali kupunguza msongamano katika Jiji la Mwanza ikiwa ni kuijenga hiyo barabara kwa njia nne, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Erick Shigongo.

**MHE. ERICK J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alikuwepo tuliposaini mkataba na mkandarasi wa Barabara ya Sengerema – Nyehunge na kwa kuwa ilitokea changamoto kidogo kwenye mkataba ule Serikali ikaamua kutafuta mkandarasi mwingine, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuwaeleza wananchi wa Buchosa wamsikie mkandarasi amepatikana na kama amepatikana ataanza kazi lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mheshimiwa Mbunge alichosema ni kweli na tulishatangaza upya hiyo barabara na sasa tupo kwenye majadiliano na mkandarasi huyo mpya ili aweze kuanza kazi na tunategemea kabla ya tarehe 30 Juni tuwe tumeanza kazi hiyo ya kuanza kujenga hiyo Barabara ya Sengerema – Nyehunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, nilikuona.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Barabara ya Mwai Kibaki inayounganisha Daraja la Mlalakuwa, linalounganisha *Kawe Round About* mpaka *Africana* itapanuliwa ili kupunguza foleni kwenye Jiji la Dar es Salaam?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, barabara alizozitaja zipo kwenye mpango wetu wa kuzijenga na itakuwa pia ni sehemu ya mipango yetu ya kupunguza msongamano wa Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo, akiangalia hata kwenye vitabu vyetu hiyo barabara alizozitaja ni barabara ambazo zinaenda kutekelezwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kakonko – Kinonko - Ruhuru – Nyakiobe – Guarama - Kabari mpaka wa Muhange, lini ujenzi wake utaanza kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, barabara hiyo ni barabara muhimu ambayo pia inaunganisha na Mkoa wa Kagera, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge,

tukishakamilisha usanifu barabara hiyo tutaanza kuijenga kwa kiwango cha kami. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay na Mheshimiwa Amandus, mtamalizia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni miaka mitatu sasa kipande cha barabara ya Mbulu – Garababi kilometa 25 mkandarasi ameitelekeza na huduma ya usafiri imekuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli ya Serikali kuhusu mkandarasi huyu ili kwenda kutengeneza hicho kipande kwa huduma ya kwanza ile ya barabara ya udongo na baadaye mradi wa lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, barabara hii tayari ina mkandarasi na alishaanza kazi na nimhakikishie Mbunge na wananchi wa Mbulu tayari Serikali imeshamlipa sehemu ya malipo aliyokuwa anayadai. Kwa hiyo, nimwagize Meneja wa Mkoa wa Mara kuhakikisha kwamba anamwimiza mkandarasi arudi *site* na kuanza kuijenga na hasa yale maeneo yote yamekwama hasa zile *diversion* ili kusiwe na mkwamo wa usafiri katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amandus.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru na tunaishukuru Serikali kwa kuipandisha hadhi kipande cha barabara kutoka Kilimarondo kwenye Lumesule, ni nini mpango wa Serikali kujenga barabara ya kutoka Kilimarondo – Bondo – Nachingwea kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ikishapandishwa hadhi kwanza ni kuijenga na kuiweka katika

barabara ambazo zina hadhi ya *TANROADS* na baada ya hapo barabara hiyo itasanifiwa ikiwa ni mpango wa kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, kwanza kutoka kwenye kiwango ilichokuwa cha *TARURA* lazima tuipandishe iwe kwenye viwango vya *TANROADS,* halafu tuisanifu kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa ni swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika Mbunge wa Njombe Mjini, swali hili litaulizwa na Mheshimiwa Neema Mgaya.

Na. 269

**Mpango wa Ujenzi wa Chuo cha Utalii – Njombe**

**MHE. NEEMA W. MGAYA K.n.y. MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** Aliuliza: -

Je, lini mpango wa ujenzi wa Chuo cha Utalii katika Mji wa Njombe utaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hili, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** Alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mpango wake wa kuimarisha utoaji huduma katika sekta ya utalii na ukarimu nchini, imeendelea kuimarisha Chuo cha Taifa cha Utalii *(NCT)* kwa kununua nyenzo za kisasa zaidi za ufundishaji pamoja na kufungua kampasi za chuo hicho katika maeneo mbalimbali nchini ili kusogeza huduma za chuo hicho karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali za kufungua kampasi mpya ambapo Wizara imepata eneo la takribani ekari

27 katika Kijiji cha Ikisa, Kata ya Uwemba, Halmashauri ya Mji Njombe. Aidha, hati ya umiliki wa eneo hilo tayari imepatikana na Wizara inatarajia kuanza ujenzi wa kampasi hiyo hivi karibuni kadiri fedha zitakavyopatikana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa Wizara ndiyo mpo kwenye mchakato wa kutegemea kupata fedha ili muanze kujenga; na kwa kuwa kuna taasisi nyingi sana ambazo zinalitaka hilo eneo ili kuweza kuliendeleza. Je, mpo tayari kuliachia hilo eneo tukafikiria kuwapa hizi taasisi nyingine kwa kuwa ninyi bado hampo tayari?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA, NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali inaendesha shughuli zake kwa mipangilio na hivyo kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, wakati wowote tunaenda kuanza ujenzi na hatuwezi kuliachia hilo eneo kwa ajili ya taasisi nyingine kwa sababu tayari tulishaliingiza kwenye mpango wa kuliendeleza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, nilikuona

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza tunaishukuru Serikali kwa kuanza kujenga Chuo cha Utalii katika Mkoa wa Iringa, lakini sasa ninaona kimesimama. Je, ni lini ujenzi huo utaendelea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA, NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa mwenyekiti, Chuo cha Utalii tawi la Iringa tayari kimeshaanza kujengwa na kwa sasa kupitia bajeti hii itakayoanza hivi karibuni

chuo kile kinaenda kuendelezwa ujenzi wake ili kikamilike haraka kwa ajili ya wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kavejuru.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana; Mkoa wa Kigoma umejaaliwa kuwa na vivutio vingi vya utalii tukiwa na mbuga ambazo zina wanyama wa pekee *chimpanzee,* Gombe na Mahale na vivutio vingine. Je, Serikali iko tayari kujenga kampasi ya chuo cha utalii katika Mkoa wa Kigoma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kwa sasa tunajaribu kuendelea kufanya tafiti ya maeneo ambayo tunaweza tukawekeza vyuo vya utalii. Ninapokea ombi la Mheshimiwa Mbunge na kwamba Wizara itaenda kufanya tafiti na ikijiridhisha itaanzisha ujenzi wa chuo ambacho Mheshimiwa Mbunge ameomba kijengwe.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa niaba hiyo ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 270

**Ujenzi wa Kiwanda cha Chai Kilolo**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** Aliuliza: -

Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga Kiwanda cha Chai cha Kilolo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, Serikali kwa kutambua umuhimu wa uwepo wa Kiwanda cha Chai Kilolo imefanikiwa kuvutia uwekezaji wa kiwanda hicho na uwekezaji umefanywa na Kampuni ya HongDingXin ya kutoka China. Kiwanda kina uwezo wa kuchakata tani 20 za chai kwa siku na kitatoa ajira 120 za moja kwa moja pamoja na kutoa soko la uhakika kwa wakulima wa chai katika Wilaya ya Kilolo na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ujenzi wa kiwanda hicho umekamilika na tayari wameshaanza majaribio tangu tarehe 28 Aprili, 2025, mara baada ya majaribio hayo kukamilika, tunaamini mpaka sasa watakuwa wameanza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kuvutia wawekezaji walioweza kujenga kiwanda kile. Ni ukombozi mkubwa sana kwa Wana-Kilolo. Pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kiwanda hiki ulitakiwa uende sambamba na ujenzi wa kiwanda cha sukari ambacho kinatengenezwa na watu wa *TEMDO*. Sasa ni lini Serikali itapeleka mitambo ya kuchakata sukari ili iweze kusimikwa katika eneo ambalo lilishaoneshwa pale Mahenge kama ambavyo ilikuwa ahadi ya Serikali na Wizara hii kwenye bajeti ya mwaka jana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Wilaya ya Kilolo ni wazalishaji wakubwa sana wa matunda lakini matunda mengi yanaoza kutokana na kwamba hakuna kiwanda kinachoweza kuyachakata.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvutia uwekezaji wa angalau kiwanda kimoja kwa ajili ya kuchakata matunda ili kuongeza thamani na kuwafanya Wananchi wa Kilolo waweze kunufaika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, kwanza, ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Justin Nyamoga kwa kazi kubwa nayofanya kufuatilia na kuhakikisha hiki kiwanda kinajengwa pale Kilolo maana kilikuwa ni kilio cha Wana-Kilolo kwa muda mrefu baada ya yale mashamba ya chai ambayo yalikuwa yametelekezwa na sasa haya ni matokeo ya ufuatiliaji wa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maswali yake mawili ya nyongeza; Serikali inatekeleza ahadi zake na ndiyo maana hata ujenzi huu wa kiwanda hiki cha chai ni utekelezaji wa ahadi zilizowekwa na Serikali kutipitia bajeti tunayokamilisha mwaka huu wa fedha wa 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye suala la Kiwanda cha Sukari pale Mahenge, ninajua wakulima tayari nao wameshalima miwa kama ambavyo kwenye chai kule Kilolo. Kwa hiyo, tunawahakikishia katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2025/2026, tumeweka bajeti hiyo kwa ajili ya kukamilisha kiwanga kile kinachosanifiwa na *TEMDO* na kitaenda kufunga pale Mahenge ili na wao pia waweze kunufaika na uwepo wa miundombinu hii wezeshi ya viwanda ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshasisitiza kuhakikisha sekta binafsi inakuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, ni kweli Kilolo ni moja ya maeneo ambayo yanalima mazao mengi ikiwemo matunda, chai na mbogamboga. Tayari Serikali ina mpango mahsusi wa kuendeleza sekta ya matunda na mbogamboga na tayari Kilolo, pale Ilula kuna kiwanda kile cha Dabaga ambacho kinachakata nyanya ili kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno. Hali kadharika tutaenda kufanya kazi kuhakikisha tunaleta viwanda vingine zaidi vya kuongeza thamani matunda kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge umesema ili kupunguza upotevu wa matunda ambayo yanakosa kuongezwa thamani ili kuendeleza sekta ya kilimo na matunda katika Jimbo la Kilolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga kiwanda cha kuchakata madini ya chumvi katika Mji Mdogo wa Nangurukuru ili kuwasaidia wazalishaji wa chumvi wa Mkoa wa Lindi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, kwanza na mimi ninachukua nafasi kumpongeza Mheshimiwa Ndulane kwa kufuatilia sekta hii ya chumvi kule Lindi na mahsusi kule Kilwa, Nangurukuru na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuvutia wawekezaji na tayari tunao wawekezaji wengine wameshaonesha nia ikiwemo wa ndani pamoja na taasisi zetu ikiwemo Magereza ambao wanaendelea kuchakata chumvi ili kuongeza kipato na thamani ya madini haya ya chumvi katika maeneo tofauti ikiwemo kwa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, na kwake tutaendelea kuvutia wawekezaji ili waje pale Nangurukuru ili kuweka viwanda hivyo vya kuongeza thamani ya chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, nimekuona.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile Kiwanda cha *MUTEX* - Musoma Serikali ilipokibinafsisha kwa *private sector*, haikuweza kuwalipa wale wananchi au watumishi mafao yao.

Je, ni lini sasa Serikali itatimiza hiyo adhima ya kuwalipa ili waweze kuendelea na maisha yao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, pia ninampongeza Mheshimiwa Vedastus Manyinyi kwa sababu naye amekuwa akifuatilia sana pamoja na viwanda vingine lakini hiki Kiwanda cha *MUTEX*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maeneo ambayo Serikali imeweka msisitizo ni kuona namna gani moja, kuona namna ya kufufua viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo vimetelekezwa na wawekezaji hawa, laikini pili, kuangalia mafao ya wale watumishi au waliokuwa wafanyakazi kwenye viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalifanyia kazi, kuona wale ambao walikuwa na madai kwenye viwanda hivi ambavyo vilibinafsishwa na havijaendelezwa ili wapete haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tuhakikishe ni namna gani ya kufufua viwanda hivyo ili viendelee kutoa ajira na kuongeza

thamani na malengo ya kiwanda kama *MUTEX* kwenye sekta ya pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ahsante. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 271

**Mradi wa Magadi Soda Engaruka**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza: -

Je, upi mkakati wa Serikali kuhakikisha Mradi wa Magadi Soda wa Engaruka unakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha mradi huu unakamilika, Serikali inatekeleza mkakati wa utekelezaji wa mradi ambapo iliutangaza mradi huo tarehe 30 Disemba, 2024 na kampuni 28 za ndani na nje ya nchi zilionesha nia ya kuwekeza katika mradi huo. Hadi mwisho wa zabuni tarehe 24 Februari, 2025 ni kampuni ambazo ziliwasilisha zabuni za kushirikiana na Shilika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua inayoendelea ni kufanya upekuzi *(due diligence)* ili kujiridhisha kampuni hizo kama zitakidhi vigezo zitapewa tuzo *(awards)* ya kutekeleza mradi huo kwa kushirikiana na *NDC*. Mpango huo uliopo baada ya kutoa tuzo na kusaini mikataba, utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza ndani ya miezi 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mradi huo hadi sasa shughuli zifuatazo zimefanyika: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tumeanza kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mradi na faida zake, lakini pili, kufanya utafiti wa awali wa magadi soda na utafiti wa kina wa magadi uliohusisha uchimbaji wa mashimo 16 ya utafiti. Pia kufanya upembuzi yakinifu na kufanya utafiti wa athari za mradi kwa mazingira na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi tulifanya uthamini na kulipia fidia ya zaidi ya shilingi milioni 5.8 ambazo zimelipwa kwa wananchi ili kupisha huo mradi. Pili, tumelipa ada za leseni za mradi huo, zaidi ya shilingi milioni 408 na tumeshautangaza mradi huo kama nilivyosema kwa lengo la kupata wawekezaji. Aidha, Serikali inaendelea na hatua mbalimbali za kuhakikisha miundombinu ya barabara, maji na umeme inakamilishwa ili kuwezesha utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Seif Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Mradi huu wa Magadi Soda wa Engaruka ni moja kati miradi ya kimkakati na ni mradi muhimu sana kwa ajili ya kutuongezea ajira pamoja na fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa zilizopo, wawekezaji wengi wanavutiwa kuwekeza kwenye mradi huu lakini changamoto kubwa ni ukosefu wa miundombinu sahihi inayoelekea kwenye mradi; Barabara ya Selela – Engaruka ni mbovu sana lakini hakuna maji wala umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upi mkakati wa Serikali sasa kuhakikisha Wizara hizi zinasomana ili miundombinu hii iweze kujengwa kwa haraka? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, kwanza, ninachukua nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Zaytun Swai kwa kuendelea kufuatilia mradi huu muhimu sana. Kama alivyosema mwenyewe, kweli ni wa kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutekeleza hii miradi ya kimkakati kama ambavyo alianza kwenye ule Mradi wa Liganga na Mchuchuma na sasa tunaenda kutekeleza Mradi huu wa Magadi Soda kwa sababu mradi huu unasaidia ukuaji wa viwanda vingi na utekelezaji wa mkakati ule mkubwa unganishi wa Maendeleo na Viwanda *(Integrated Industrial Development Strategy)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mkakati huu mkubwa, moja ya mradi ni huu wa Magadi Soda. Kama nilivyosema, tumeshaanza kwanza kulipa fidia na kutoa elimu kwa wananchi ili kupisha mradi. Zaidi sasa nimesema kwenye jibu langu la msingi, tunachoenda kufanya sasa ni kuanza kuweka bajeti ya kuweka miundombinu wenzeshi ikiwemo hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ametaja; barabara, maji, umeme na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mradi huu ili utekelezwe ni lazima haya yote yakamilike. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake na nia njema ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunaenda kutekeleza mradi huu kama ambavyo tumeanza kutekeleza miradi mingine ili isaidie kupunguza uagizaji wa bidhaa au malighafi hii ambayo inatumika kwenye viwanda vingi ikiwemo viwanda vya vioo, sabuni, rangi, karatasi, kusafisha mafuta ya petroli na kadhalika, ambayo tunatumia fedha nyingi sana za kigeni kuagiza kutoka nje wakati tunayo hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, tuna swali la Mheshimiwa Abdi Hija Mkasha, Mbunge wa Micheweni. *(Makofi)*

Na. 272

**Kuboresha Kituo cha TEHAMA Micheweni**

**MHE. ABDI HIJA MKASHA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukiboresha Kituo cha TEHAMA kilichopo Wilaya ya Micheweni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa niaba ya Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* ilitekeleza mradi wa ujenzi wa vituo 11 vya TEHAMA, Unguja na Pemba ambapo kwa kila wilaya kimejengwa kituo kimoja kwa madhumuni ya kuwapa fursa wananchi wa Zanzibar kujifunza na kutumia TEHAMA kwa ajili ya manufaa yao wenyewe ili kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kiutamaduni. Kituo cha TEHAMA Sokoni kilichopo Wilaya ya Micheweni ni miongoni mwa vituo hivyo ambapo kinaendelea kutoa huduma kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali kuhusu kukiboresha kituo husika kilichopo katika Wilaya ya Micheweni, inaashiria kuwa ipo changamoto. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi itafanya tathmini ili kujua mahitaji halisi ya kituo hicho kwa lengo la kufanya maboresho yanayohitajika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdi Hija Mkasha.

**MHE. ABDI HIJA MKASHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza (a) na (b) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imekiri kuwepo kwa changamoto katika kituo kile; je, ni lini itaharakisha kwenda kufanya tathmini hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa katika kituo kile kuna vijana ambao wanajitolea, je, Serikali ipo tayari kuwafanyia mpango angalau wa kupata posho ya kuweza kujikimu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Abdi Mkasha kwa kufuatilia maslahi ya vijana ambao wako pale tayari wanafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, tayari sisi kama Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Tanzania Bara tulishafanya sehemu yetu kupitia *UCSAF* na tayari tumeshakabidhi kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Hivyo, ninapenda tu kukwambia kwa sababu tunafanya kwa ushirikiano basi nitawasiliana na wewe na kuona namna njema ya kukukabidhi kwa wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili waweze kufanya haya wote mawili; kuharakisha katika maboresho, lakini vilevile kuangalia maslahi ya vijana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar, nilikuona.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa kituo hiki wamekuwepo vijana na wamejitolea kwa muda mrefu na kwa kuongeza kasi ya kuwapatia vijana mafunzo na kuzingatia maendeleo makubwa ya teknolojia, je, Serikali ya SMZ pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haioni haja ya kukaa pamoja kuwapatia ajira za moja kwa moja

hawa vijana ili kuwapa moyo wa kufanya kazi kwa bidii zaidi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninashukuru sana kwa swali zuri ambalo linaendelea kukazia maslahi ya vijana kuona sasa wanapata ajira. Tunafahamu taratibu za ajira za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilivyo na sisi kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuna Sekretarieti ya Ajira na tuna Wizara ya Utumishi, lakini haya yote kwa sababu tayari wako ndani, vigezo na masharti vitazingatiwa kuona namna gani wanaweza kupatiwa ajira. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Mhata, nimekuona.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwenye Tarafa ya Nakopi, Kata ya Napacho, Kampuni ya Minara Tanzania ilipewa kazi ya kusimika minara katika eneo hilo, jambo ambalo sasa ni mwaka mmoja huo mnara haujasimikwa. Changamoto kubwa ni mawasiliano ya kufika katika eneo ambalo mnara unatakiwa kujengwa.

Je, Serikali iko tayari kuisaidia hii Kampuni ya Minara Tanzania wakatengeneza miundombinu ya barabara ili waweze kufika katika eneo ambalo limekusudiwa kujengwa mnara huo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya kuhusu barabara ya kufika katika maeneo ya ujenzi wa minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara tayari tumeshafanya mawasiliano na wenzetu wa TAMISEMI kuona *TARURA* inaweza kuingilia kati na kuona namna njema ya kusaidiana na hawa watoa huduma ili waweze kutengenezewa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wakati mwingine wananchi wanaweza wakatoa nguvu kazi kama inawezekana kulingana na jiografia ili kuona minara hii inajengwa na maeneo hayo yanaweza kupitika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunamalizia Wizara ya Maji, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, aulize swali lake.

Na. 273

**Mradi wa Maji Ziwa Victoria – Kishapu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** Aliuliza: -

Je, lini usambazaji wa maji ya Ziwa Victoria katika Kata za Mondo, Busangwa, Sekebugolo na Mwasubi - Kishapu utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** Alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, Serikali imekamilisha usanifu wa kina wa mradi wa kutumia maji ya Ziwa Victoria kwenda kwenye Kata za Wilaya ya Kishapu ikiwemo Kata za Mondo, Busangwa, Sekebugolo na Mwasubi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mradi huo ni kutatua changamoto ya huduma ya maji katika kata hizo ambapo kiasi cha shilingi bilioni 16.1 kinahitajika. Kwa sasa Serikali inaendelea na utafutaji wa fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo. Aidha, kwa sasa huduma ya maji inapatikana kwa baadhi ya maeneo ya kata hizo kupitia visima vya pampu za mkono 12, Bwawa la Sekeididi pamoja na mtandao wa mabomba wa zamani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, kwanza, ninaomba niipongeze Serikali kwa kazi kubwa inayofanya ya usambazaji wa maji katika Wilaya yangu na Jimbo langu la Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ninapongeza usanifu wa kina uliofanyika ambao una thamani ya jumla ya shilingi bilioni 16.5 ambayo kimsingi itakwenda kutatua tatizo la maji katika kata hizi tatu.

Swali, je, Serikali iko tayari sasa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kuhakikisha kwamba inatekeleza miradi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ninaiomba Serikali iweze kunihakikishia kama itaweza kufanya usanifu wa kina katika Kata ya Masanga, Kata ya Mwamalasa pamoja na Kata ya Kiloleli. Hizi ni kata ambazo zina changamoto kubwa ya maji na bahati zuri yako matoleo ya Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria. Je, Serikali iko tayari kufanya upembuzi wa kina ili mradi sehemu hii na yenyewe iweze kupata huduma ya maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na pia ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu. Ninampongeza sana kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kwa Wana-Kishapu. Hakika Wanakishapu wamepata mwakilishi mahiri kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata usanifu huu uliofanyika wa kuhakikisha kwamba tunaangalia huduma ya upatikanaji wa maji na tukaja na hii *figure* ya shilingi bilioni 16.1, ni kwa sababu ya umahiri wa Mheshimiwa Butondo kwa kushirikiana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, lakini vilevile katika bajeti ya mwaka 2024/2025 tulitenga shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya miradi ndani ya Kishapu, lakini katika bajeti hii pia Mheshimiwa Butondo

tumemuongezea kwa ajili ya wananchi wake wa Kishapu shilingi bilioni 1.77, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba miradi mingine inaendelea kutekelezwa, lakini nimtoe hofu, Serikali iko tayari kutenga fedha hizi katika bajeti ijayo ili kuhakikisha kwamba sasa tunaenda kutekeleza mradi huo kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kata za Kiloleni, Masanga pamoja na Mwamalasa. Mheshimiwa Mbunge nikutoe hofu, wewe mwenyewe umesema kwamba kuna Mradi wa Ziwa Vikroria kazi iliyobaki pale ni kufanya usanifu na Serikali tuko tayari kwenda kufanya usanifu, lengo ni kwamba wananchi wako wapate huduma ya majisafi na salama kutoka Ziwa Viktoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nimewaona, Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma, Mheshimiwa Vincent Mbogo na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji Mogitu Gehandu, awamu ya kwanza imekamilika na awamu ya pili ambako sehemu kubwa ya Kata ya Gehandu imepata maji. Lini awamu ya tatu itakamilika ili maji yaweze kufika Gidabwanja, Marega, Mwanina, Milongori na eneo la Alosabida?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana kaka yangu mhandisi kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya na nimuombee kwamba mambo yake yaende vizuri, lakini kwenye mradi wa awamu ya kwanza ni kazi yake kubwa, awamu ya pili ni kazi yake kubwa ambayo ameifanya kwa kushirikiana na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi katika utekelezaji wa Ilani ya CCM, lakini vilevile nimuahidi, huu mradi wa awamu ya tatu, sisi ni kipaumbele cha Serikali kutokana

na maombi yako kwa ajili ya wananchi wako. Nikutoe hofu katika bajeti hii inayokuja tunaenda kuhakikisha kwamba mradi huo unatekelezwa kwa awamu ya tatu ilimradi wananchi wa eneo lako wapate huduma ya majisafi na salama, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vincent.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nina swali dogo moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Ntemba, Kata ya Kate hakina maji kabisa, lini Serikali mtapeleka maji katika Kijiji cha Ntemba na kuwasambazia wananchi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti yetu ambayo Mheshimiwa Waziri wa Maji Jumaa Hamidu Aweso jana aliiweka mbele ya Bunge lako Tukufu, imeangalia sana Jimbo la Nkasi ambako Mheshimiwa Mbunge anatoka na ni lengo la Serikali kutokana na Ibara ya 100 ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali itahakikisha kwamba inafikisha miradi ya maji vijijini ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kuenzi na kuhakikisha kwamba ajenda ya kumtua mama ndoo kichwani iliyoasisiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inaonekana kwa vitendo. Lengo ni kwamba ionekane pale ambako watu wanachota maji katika maeneo ya makazi bila kuwa na changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mbunge tutafanyia kazi kwa umakini mkubwa sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi wa maji ambao Serikali ilitenga zaidi ya shilingi milioni 950 kwenye hii Kata ya Ndanda mpaka utakapokuwa umekamilika, lakini mradi huu unapokwenda kuhudumia Vijiji vya Liputu, Tuungane, Mpoora; Njinga pamoja na Majengo.

Swali, wakati wa usanifu wa mradi huu, walikuwa hawajatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa chujio na wananchi wa kata hiyo kwa kipindi fulani hasa wakati mvua zinanyesha wanapata maji machafu.

Je, Serikali haioni haja ya kutenga pesa kwa ajili ya kujenga chujio ili kuwaondolea adha wakazi wa Ndanda waweze kupata majisafi, salama na ya kutosha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Cecil Mwambe, ni ushauri mzuri sana kwa Serikali, na lengo la Serikali ni kwamba wananchi wapate majisafi na salama na kama wananchi wanapata maji ambayo hayaridhishi na *solution* kama ni kuweka chujio, Serikali haitochelewa kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kwamba tunaenda kujenga chujio ili wananchi wapate huduma ya maji yaliyo safi, salama na toshelevu na yenye bei ambayo inakubalika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, Mradi wa Maji Wilaya ya Chemba, Kelema Maziwani pamoja na Ovada, vifaa tunavyo, lakini pili miundombinu yote imekamilika na mabomba tunayo, tunahitaji shilingi milioni 214 ili tukamilishe usambazaji wa maji kwa wananchi

wetu. Je, ni lini mtatupatia fedha hizi ili wananchi wetu waweze kupata huduma hii bora ya maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na nimshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Kunti kwa kuwasemea Wananchi wa Kata ambazo amezitaja, lakini pia kwanza ametambua Serikali tayari imeshafanya hatua ya kwanza, mradi umeshaanza tayari bomba zimeshakuwepo pale, maana yake ni kwamba zaidi ya 70% imeshafanyika. Kwa hiyo 30% kama ambavyo anaomba hizi fedha shilingi milioni 200, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan haiwezi kushindwa kutoa shilingi milioni 200 ili kukamilisha mradi huo na wananchi wake wapate huduma ya majisafi na salama. Mheshimiwa Mbunge ninakuahidi hilo tunalichukua na tunaenda kulifanyia kazi kwa uzito stahiki, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ninashukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge, na hapo ndipo mwisho wetu wa maswali kwa siku ya leo. Mheshimiwa...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nimesimama kwa jambo lililotokea leo mapema nikirejea swali namba 264 ambalo lilikuwa linazungumzia kuhusiana na ujenzi wa uzio kwa shule za msingi, na majibu ya Serikali yameonyesha juhudi ambazo inazipelekea hasa kwa kuanza kwa kujenga shule za watoto wenye mahitaji maalumu (shule maalumu) kulingana na upatikanaji wa fedha na wakaonyesha kwamba wataendelea kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wewe mwenyewe ni dhahiri umeona idadi kubwa sana ya Wabunge waliosimama kuonesha ukubwa wa uhitaji wa ujenzi wa uzio kwenye shule zetu na hasa za mijini, kama swali la msingi ambalo nimelielekeza. Kuna muingiliano mkubwa sana wa watu, vyombo vya moto na shughuli mbalimbali za kijamii, ambazo zinapelekea kupunguza umakini na usikivu wakati wa kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali imeonesha inaenda kwa kadiri fedha zinavyopatikana na imeelekeza kwenye halmashauri, na halmashauri nyingine hazina fedha, kwa mfano Halmashauri ya Mji wa Tarime. Tuna shule ambazo ziko katikati ya mji, Shule ya Msingi Azimio, Mapinduzi; Sabasaba, ukienda kule Lebu, Tuna na Buguti na nina imani na kwingine kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini Serikali haioni kwamba kuna haja ya kukaribisha *private sectors* kupitia *PPP*, ili waweze kujenga uzio na upande wa huku kwa nje waruhusu shughuli nyingine ziendelee ambazo zilikuwa zimeweka uzio, lakini zimehamishwa, kwa mfano maduka na ofisi, kama ilivyo *Pamba Secondary* ya Mwanza na kama ilivyo Benjamin Mkapa ya Kariakoo. Tuna imani kama Serikali ikiona kuna tija ya hivi, kwa sababu hakuna upatikanaji wa fedha, ili kuweza kuimarisha usalama na watoto waweze ku-*concentrate* kujifunza, waruhusu *private sectors* waweze kujenga huu uzio kwa mikataba maalumu ambayo itatoa usalama, kujenga uchumi, pia na ku-*generate* uendeshaji wa shule zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikasema, kwa ukubwa wa hili nikataka mwongozo wako, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kukaribisha *private sector* waweze kushughulika na hili jambo kupunguza dhahama hii ya ukosefu wa uzio kwenye shule zetu za msingi hasa zilizopo mjini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Esther Matiko amesimama kwa ajili ya kuomba mwongozo kutokana na kujitokeza kwa wingi kwa Wabunge kwenye uhitaji wa uzio wa shule zetu za msingi, lakini maeneo mengi nchini kama ambavyo

leo mmesikia hapa, wengi wameuliza swali hili na huu ni ushauri mzuri, ninaamini Serikali inafanya jitihada kubwa sana.

Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba, Serikali baada ya kuupokea ushauri huu mimi hapa kwangu ninaomba na wao wazingatie kuona ni namna gani wataweza kufanya, lakini bila kuharibu maslahi mapana ya Taifa letu.

Kwa hiyo, ushauri huu wa kuwa na ushiriki wa *private sectors* ama hawa watu binafsi kwa mpango wa *PPP* siyo mbaya, lakini Serikali iangalie namna bora ambayo haitoleta athari katika Taifa letu. Huo ndiyo mwongozo wangu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo tuna matangazo mawili; kwanza kwenye tangazo la Kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo nje ya Dodoma kwa shughuli za kikazi kuanzia tarehe 8 Mei, 2025 wakati hayupo Mheshimiwa *Captain* Mstaafu George Huruma Mkuchika, atakaimu nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa *Captain* Mstaafu George Huruma Mkuchika atakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali hadi hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaporejea au Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati atakaporejea. *(Makofi)*

Tangazo la pili, ni tangazo la wageni waliopo asubuhi hii; kuna wageni waliopo kwenye Jukwaa la Spika, kuna wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ndugu George Msafiri, mjasiriamali kutoka Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine waliokaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, ni wageni wawili wa Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge na Waziri wa Maji, Mheshimiwa Zainab Abdallah ambaye ni mke wa Mheshimiwa na Mkuu wa Wilaya ya Muheza. Mheshimiwa Zainab Abdallah ambaye ni mke wa Mheshimiwa wetu, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna Mhandisi Ngwisa Mpembe, Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Maji. Mwenyekiti wetu wa Bodi ya Taifa ya Maji, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira kutoka Shirika la Kimataifa la *Women Political Leaders* na Shirika la *Omuka Hub* wakiongozwa na Ndugu George Gyedu, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 32 wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, ni Kikundi cha Kwaya cha Beroya cha Kanisa la Adventista Wasabato kutoka Mburahati Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Masau Bwire, karibuni sana Wakakwaya wetu. *(Makofi)*

Tuna wageni 11 wa Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Naibu Waziri wa Uchukuzi ambao ni Wanachama wa *Red Cross* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha, hawa ni Wapigakura wake kutoka Kojani Pemba wakiongozwa na Katibu wa Jimbo, Ndugu Tamim Ali Omary. Wapigakura wa Mheshimiwa wetu Naibu Waziri, ninaamini mko naye vizuri hamtomuangusha miaka mitano ijayo, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 57 wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, wakulima wa pilipili kutoka mikoa mbalimbali nchini Tanzania wakiongozwa na Ndugu Judith Jonaro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Viongozi wa Shirika Liliso la Kiserikali la *TAWEN* kutoka Mbozi, Mkoani Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 58 wa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, wapigakura wake kutoka Kata ya Laiseri Wilaya ya Kiteto, Mkoani Manyara. Wapigakura wetu wa Mheshimiwa Edward, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Wakili Livino Haule, Mwanasheria wa Chuo cha Uhasibu Arusha. Mgeni wetu wa Mheshimiwa Kamonga, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine 16 wa Mheshimiwa Kamonga ni wanafunzi wa Ndaki ya Biashara ya Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Wanafunzi wetu wa Mheshimiwa Kamonga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Ally Juma Makoa, marafiki zake aliosoma nao Shule ya Msingi Mpalangwi kutoka Kondoa, Mkoani Dodoma. Hongera Mheshimiwa Ally Makoa kwa kuwakumbuka wanafunzi wenzio mliosoma zamani, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 29 wa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, walimu wanne na wanafunzi 25 wa Shule ya Msingi Paradigms kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Khalifa Salum Suleiman, wapigakura wake kutoka Tunguu, Zanzibar. Wapigakura la Mheshimiwa wetu Khalifa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ambaye ni Mhandisi Sadara Hamza, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Sengerema *(SEWASA)*, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tuna viongozi 18 wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo cha Uhasibu *(TIA)* Kampasi ya Mbeya. Wanafunzi wetu kutoka huko Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wafanyakazi wawili wa Shirika Lisilo la Kiserikali la Kiswahili Nguzo ya Umoja wa Afrika, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 40 wa Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Kampasi ya Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wetu wote, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Katibu, tuendelee.

**NDG. BAKARY KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu kwenye hoja za Serikali, Wizara ya Maji.

Kwa siku ya leo wachangiaji ni wengi, kwa hiyo kila mchangiaji atachangia kwa dakika tano, tutapiga kengele moja, tunawaomba sana mzingatie muda na mfupishe mazungumzo. Muongee yale mambo muhimu zaidi kuliko yote.

Tunaanza na Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mheshimiwa Kwagwila Reuben Nhamanilo ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini kipekee kabisa nimpongeze sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu ameleta tafsiri sahihi ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ningepewa nafasi ya kuchagua Mawaziri watatu bora katika Bunge hili, basi Mheshimiwa Jumaa Aweso angekuwa miongoni mwao, na amejaribu kuheshimisha vijana kwa kuonesha uwezo wao. Mheshimiwa Rais kama itampendeza, ninaamini anakwenda kushinda Ubunge kule Pangani, abaki hapa ili aendelee kutekeleza matakwa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Mtwara hususani Newala, Tandahimba na Nanyamba ni watu ambao tumepata shida ya maji kwa muda mrefu na tumekuwa na Mradi wa Maji wa Makonde ambao takribani tangu tumepata uhuru haukuwahi

kutengewa japo shilingi bilioni moja. Lakini kwa dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais ule mradi leo tunavyozungumza wakandarasi wako *site* na ametoa fedha shilingi bilioni 84.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu Tandahimba, katika mambo ambayo tunafikiria kuyafanya sisi Wamakonde kuna lugha tunaita *kumbamba ndija* yaani kitu kinajaa halafu unaongeza kujazia. Kwa yaliyofanywa sekta ya maji na Rais Samia kupitia Jumaa Aweso hatuna sababu ya mwaka 2025 kupoteza kura hata moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunayo miradi ya maji ambayo ilikuwa imesuasua kwa muda mrefu. Tuna Mradi wa Maji wa Mkwiti ambao leo tunavyozungumza mkandarasi ameshalipwa fedha na kilichobaki sasa ni kumaliza vioski vidogo ili maji yaanze kutoka, na kwenye hili Mheshimiwa Aweso kuna kamgogoro kadogo ambacho ninakuomba sana wakati unafanya hitimisho uone namna unavyoweza kuliweka hili jambo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo deni la milioni nne la watu wa Makonde kuwadai watu wa *RUWASA*. Kumbuka ule mradi bado mkandarasi hajaukabidhi kwa wananchi na wakati anafanya *testing* ilikuwa ni lazima wananchi wayaone maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumekuwa na shida maji hayajazwi pale kwenye tenki, kwa sababu watu wa Makonde wanadai *RUWASA* shilingi milioni nne. Kwa hekima zako na busara zako ninaamini tukishahitimisha hii bajeti, kwa maana tunakwenda kuipitisha ili jambo Wizara mlichukue na mlimalize. Mmetoka kutoa taarifa hapa kwamba Mheshimiwa Rais anayafuta madeni ya maji, basi pamoja na hayo madeni hili unaliweza Mheshimiwa Aweso. Nione unalichukua kama wewe na hili jambo liishe ile wale watu wa Mangombyam wale watu wa Nanjangam wale watu wa Ngunjam wale watu wa Namindondim wale watu la Mkwitim wale watu wa Likolombe na wale watu wa Kidoo, waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi ambao Mheshimiwa Waziri atusaidie. Mradi wa Maji wa Mtopwa – Orodaleo. Ule mradi

uko kwenye michakato yenu, sasa niombe muinasue kwa sababu wananchi wanaufahamu vizuri na ni mradi mkubwa wenye thamani zaidi ya shilingi bilioni tisa, ambao kama mtaufanya uende kwa haraka unakwenda kutupatia matumaini na maongezeo ya kura za Mheshimiwa Rais kwenye uchaguzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mradi huu wa maji tunaozungumza wa Makonde mkandarasi amesha-*raise certificate* anahitaji shilingi bilioni 3.1 aweze kuendelea na kazi na ule mradi unalisha Newala, unalisha Tandahimba, unalisha na Nanyamba muone namna mnavyoweza ku-*fast track* na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili mkandarasi huyu alipwe fedha mambo yaweze kukimbia.

Mheshimiwa Waziri, tunao mradi ule pia wa Nanyuila – Maundo mkandarasi nae ame-*raise certificate* bado hajalipwa na mradi ule pia unaenda kuhudumia kata zaidi ya tano, Kata ya Lukokoda, Kata ya Kwa Nyama, Kata ya Maundo, Kata ya Mchichira na Kata ya Mnyawa. Niwaombe sana muone namna mnavyoweza kukimbizana na haya ma-*certificates* ili waweze kulipwa wananchi wale wanataka matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na bahati njema Mheshimiwa Aweso hii umeliweza kwa Tandahimba leo ukienda ilivyo Kitama watu wanapata maji kwenye vijiji vyao, ukienda Mkundi watu watapata maji kwenye vijiji vyao, hata visima hivi ulivyovichimba vitano mmefanya kazi kubwa kwenda kuweka na *solar panels* watu wanapata maji. Niwaombe sana, sana, sana pelekeni fedha ili wakandarasi wamalize miradi ile ili wananchi wetu waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningane na Wabunge wenzangu kuunga mkono hoja ya kupitisha

shilingi 1,16,894,958,000 kwa ajili ya kwenda kumwezesha na kuziwezesha kazi za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye sekta hii ya maji, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mapinduzi makubwa sana ndani ya miaka hii minne kwenye sekta hii ya maji. Sisi Handeni Mjini tunampongeza sana tunamshukuru sana, lakini nitumie nafasi hii pia kukushukuru Waziri Mheshimiwa Aweso kaka yetu na mdogo wetu, sisi wenzako Wabunge tunaotoka Mkoa wa Tanga tunajivunia kujitambulisha kwamba Mheshimiwa Waziri wa Maji anatoka Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa *Engineer* Kundo, hongera sana kwa uchapakazi wako mapema sana ulifika Bwawa la Kwenkambala, mapema sana, maelekezo uliyoyaacha pale kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri na kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, yametekelezeka na ninataka niwajulishe kwamba bwawa lile kwa sasa imekamilika, Bwawa la Kwenkamba. Ombi langu kwenye bwawa hili ni kwamba tumemaliza awamu hii ya kwanza ya kulijenga bwawa sasa twende awamu ya pili ya kutenegeneza *treatment plant* na baadaye tuyapandishe maji juu ya kilele cha Mlima Mhandeni kwenye tenki la ukombozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mkubwa ambao Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameufanya Jimbo langu la Handeni Mjini ni Mradi wa Maji wa *HTM,* mradi wa kitaifa, mradi wa shilingi bilioni 171, mradi ambao toka mwaka 1974 hatukuwahi kuwa na mradi mkubwa kama huo isipokuwa Awamu hii ya Sita. Kupitia mradi huu tunayatoa maji Mto Ruvu – Korogwe tunayaleta mpaka juu ya kilele cha Mlima Mhandeni mahali ambapo tumejenga tenki kubwa. Mheshimiwa Rais ametuwezesha kujenga tenki kubwa pale, tenki ambalo yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais amefika kwenye kilele cha mlima huo na kuiweka alama ya kumaliza matatizo ya maji kwenye Mji wa Handeni. Maji yatatiririka kutoka juu ya kilele cha Mlima Mhandeni kwenye tenki la Ukombozi mpaka Kata ya Kwa Magome yataanzia pale Hedi, Kwa Magome yatakwenda Kwa

Magome – Lusanga, Lolopili – Sasioni mpaka Kolubaka kata yote ya Kwa Magome maji yatatiririka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka juu ya kilele cha Mlima Mhandeni kwenye tenki la Ukombozi ambalo Mheshimiwa Rais amelizindua maji yatakwenda mpaka Kata ya Malesi, yataanzia Malesi penyewe yatakwenda mpaka Masampata, yatakwenda Kulukole, yatakwenda kwa Madule na yatafika viunga vyote vya Kata ya Malesi toka juu ya kilele cha Mlima Mhandeni maji yatatiririka. Maji yatatiririka kutoka tenki la Ukombozi mpaka Kata ya Konje yataanzia Kiturwe yatakwenda Masalanka, Mankinda yatafika mpaka Komnazi maji yatatiririka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yatatiririka mpaka Kata ya Kwenjugo kuanzia Wandama, Kwedigongo, Ngugwini, Kwediswa mpaka Bwila kata yote ya Kwenjugo itapata maji kutoka juu ya kilele cha Mlima Mhandeni kwenye tenki la Ukombozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yatatiririka mpaka Kata ya Msasa, yataanzania Msasa shule yatapita Mazundu, maji yatakwenda mpaka Kwedeseni, yatakwenda Visenenzi na mpaka Mnazi mmoja maji yatatiririka, kazi za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, maji yatatiririka mpaka Kata ya Mlimani, yataanzia Kwa Baya yatafika kwa Sindi maji yatakwenda mpaka kwa Sahasani pale Anitakaye, maji yataririka kutoka juu ya kilele cha Mlima Mhandeni kwenye tenki ambalo Mheshimiwa Waziri unalifahamu vyema tenki maarufu tenki ambalo tumekubaliana kulipa hilo jina la Ukombozi kwa sababu Handeni Mjini tumekuwa kwenye dhiki kubwa ya maji kwa miaka mingi mpaka hapa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyokuja kutukomboa Wana-Handeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yatatiririka kutoka juu ya kilele cha Mlima Mhandeni mpaka Kata ya Kideleko, yataanzia vilima vya Bangurandekai yatashuka Lumbizi, yatashuka Kideleko yenyewe, Kampene mpaka maeneo yote ya Kata hiyo ya Kideleko maji yatatiririka. Maji yatatiririka kwenye viunga ya Kata ya Vibaoni, Chanika na Mdoe pale mjini pote soko la zamani kote maji yatatiririka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mheshimiwa Hassan Zidadu kingu ajiandae.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika nchi yetu na hasa katika Wizara hii ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri wa Maji Mheshimiwa Jumaa Aweso kwa namna ya pekee anavyopambana katika mikoa yetu na majimbo kuhakikisha wananchi wanapata maji katika kumsaidia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan hongera sana Mheshimiwa Jumaa Aweso, wewe na Naibu Waziri wako lakini na watendaji wote wa Wizara ya Maji akiwemo dada yetu Ndugu Mwajuma hongera sana, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo nikiwa namaanisha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameibeba ajenda ya kumtua mwanamke ndoo na hata sisi tunaotokea katika Kanda ya Ziwa ameibeba ajenda hiyo kupitia Ziwa Victoria kuhakikisha wananchi wa Kanda ya Ziwa wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamaanisha hivyo ukienda katika Mkoa wa Mara sisi Wana-Mara tumepata miradi mikubwa na midogo. Katika miradi midogo ya maji tumepata miradi ya maji miradi 100 ambayo miradi ile imegharimu shilingi bilioni 35.77 itaenda kuhudumia wananchi 4,667 hii ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anatupenda sana katika ndani ya miaka minne hiyo kazi imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepata miradi mikubwa ya maji, tumepata mradi wa Mgango – Kiabakari wa shilingi bilioni 70 mradi ule unaenda kuhudumia wananchi 150,000 na kuendelea, lakini pia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kutupa mradi mwingine wa maji, ukienda pale Bunda tumepata mradi wa maji wa shilingi bilioni 10 ule mradi wa chujio la maji utaenda kuhudumia wananchi takribani 160,000 na hapa nimpongeze sana dada yetu Ndugu Ester amekuwa ni Mkurugenzi mzuri ambaye anasimamia vizuri miradi ya maji tunampongeza sana yeye pamoja na watendaji wa Bunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeendelea kupata miradi yam aji ile ambayo inaendelea kutekelezeka, tumepata miradi ya maji, maji vijijini miradi 38 na miradi hiyo tumepewa shilingi bilioni 24 na tayari shilingi bilioni 10 imeshakuja. Hiyo ni kazi kubwa na nzuri ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan chini ya Waziri makini, Mheshimiwa Jumaa Aweso unayepambana kumsaidia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeendelea kupata miradi ambayo inaendelea mpaka sasa kutekelezeka tumepata mradi wa miji 28 mradi ambao utaenda kuifanya Tarime Mjini, Tarime Vijijini lakini mpaka na Rorya wanawake wa Mkoa wa Mara kupitia mradi huo watapata maji, wanawake wa Tarime watapata maji, mama zangu wa Tarime Vijijini watapata maji. shilingi bilioni 134 Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo hakuwasahau wananchi wa Serengeti kwa kuleta shilingi bilioni 20 kwa ajili ya mirafi ya maji wanawake, wakina mama, mama zangu wa Wilaya ya Serengeti wataenda kupata maji. Hii ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kwa dhati kabisa kumtua mwanamke wa Mkoa wa Mara ndoo na hii ni utekelezaji mzuri wa Meneja wetu wa Mkoa wa Mara Meneja wa *RUWASA* kaka yangu ninakupongeza sana kwa namna ambavyo umepambana kuhakikisha unaisimamia miradi ya maji

katika Mkoa wa Mara, wanawake wa Mara watapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenu, ombi langu na ushauri wangu kwa Serikali ni kuhakikisha miradi ya maji inataklezeka kwa kuleta feda nyingi ili miradi ile iweze kukamilika tumsitie doa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyojitolea kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Mara wanapata maji, wananchi wa Tarime, wananchi wa Serengeti, wananchi wa Rorya, wananchi wa Butiama, wananchi wa Tarime Mjini, wananchi wa Tarime Vijijini, wananchi wa Bunda wanaendelea kupata maji katika kumtua ndoo mwanamama wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge ajiandae.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara hii ya Maji, lakini kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uhai leo hii tuko hapa na kuweza kuchangia katika Wizara hii.

Pili, nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kweli Mama yetu tunadiriki kusema anaupiga mwingi japo watu wakisikia kwamba tunasema anaupiga mwingi wanakasirika, lakini ukweli ni kwamba Mama anaupiga mwingi lakini hasa katika adhima yake ya kumtua ndoo mama kichwani na hii imedhihirika katika Jimbo langu la Tunduru Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Jumaa Aweso kwa kweli anafanya kazi kubwa sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Naibu Waziri wake kwa sababu anamsaidia kazi vizuri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Maji hakika wanaitendea haki Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kuzungumzia maji Tunduru Mjini, maji Tunduru Mjini na Vijijini kwa ujumla wake kwa muda mfupi huu mimi nilipoingia madarakani jumla ya shilingi bilioni 12.321 na zaidi zimetekeleza miradi ya maji ya Tunduru Mjini pamoja na Tunduru Vijijini ambapo shilingi bilioni 7.4 na zaidi imekwenda kutekeleza maji Tunduru Vijijini kwa maana ya *RUWASA,* lakini shilingi bilioni 4.8 imekwenda kutekeleza maji mjini kwa maana ya *TUWASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimshukuru sana, sana, Mheshimiwa Waziri wa Maji Tunduru Mjini tulikuwa tunachangamoto kubwa sana ya maji na kulikuwa kuna lawama nyingi za watumiaji wa maji wengine walikuwa wanapelekewa bili na wansema kwamba tumeletewa bili, lakini kwa mwezi mzima hatujaona maji lakini tumeletewa bili na maji yanaweza kutoka mara moja, mara mbili kwa mwezi ama mara tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo changamoto ilikuwa ni kubwa sana, lakini baada ya ujio wa Waziri wa Maji ndugu yangu Mheshimiwa Jumaa Aweso alipoikuta changamoto ile pale pale alichukua hatua tena ilikuwa mbele ya Madiwani pamoja na *DC* wetu mchapakazi mkubwa katika Wilaya yetu ile ya Tunduru Mjini. Pale pale alichukua hatua kwa kutoa pesa za dharura jumla ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya kwenda kuboresha miundombinu ya maji pale mjini, lakini alitoa gari kwa ajili ya kuisaidia idara ile, lakini pia alitoa pikipiki 10 mpya kwa ajili ya kuwawezesha wale wataalamu wa maji ili kwenda kutatua matatizo kwa haraka zaidi badala ya kwenda kwa mguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Aweso tunakushukuru sana, sana, sana, lakini kama haitoshi pale mjini sasa hivi tunao mradi ambao tumesaini juzi tu leo ni siku ya tatu mradi wa shilingi bilioni 3.2 ambapo *engineer* yule, *Engineer* Kiwia amekwenda amefanya utafiti na amegundua eneo lenye mwinuko mkubwa zaidi ambapo mradi

ule ukienda ukikamilika utakwenda kutatua changamoto ya maji katika kata zote saba za tarafa ya Tunduru Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaanisha kwamba mradi ule ukikamilika Kata ya Sisi Kwa Sisi itakwenda kunufaika na mradi ule Kata ya Nanjoka itakwenda kunufaika na mradi ule, Kata ya Majengo itakwenda kunufaika na mradi ule, Kata ya Nakapanya itakwenda kunufaika na mradi ule, Kata ya Mlingoti Mashariki itakwenda kunufaika na mradi ule Kata ya Mlingoti Magharibi itakwenda kunufaika na mradi ule.

Mheshimiwa Waziri lakini pia mimi nikuombe sana tena sana katika mameneja wa maji wote mjini waliowahi kupita Tunduru Mjini kwa kweli *Engineer* Kiwia anafanya kazi kubwa sana, tena sana nikuombe usituhamishie meneja huyu ndugu yangu *Engineer* Kiwia tafadhali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye maji mjini naenda maji vijijini kwa maana ya *RUWASA*, kwa kweli hapa mama ameupiga mwingi mno, mno, mno. Maji vijijini kwa maana Kata ya Namwinyu tuna mradi ambao mpaka sasa umefikia hatua ya 70%; tunao mradi kule kwenye Kata ya Namwinyu tuna mradi wa shilingi milioni 450 ambapo utekelezaji wake upo katika 70%, lakini Kata ya Kijiji cha Ulia tuna mradi wa jumla ya shilingi bilioni 1.26 ambapo wenyewe tayari umekwisha kamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kesho kutwa tu nikienda kwenye mwenge tunakwenda kuuzindua rasmi mradi ule na akina mama wanakwenda kuteke maji na hatimaye tutaimba nyimbo ya Samia, Samia, Samia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge na Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo wajiandae.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nataka nimpongeze Mheshimiwa Rais na kumshukuru sana kwa namna

ya pekee ambavyo mmendelea kutupa miradi mingi ya maji ambayo kwa kweli nikuombe Mheshimiwa Waziri uandae utaratibu ili Mheshimiwa Rais aje afungue Mradi wa Maji Magu ambao umenufaisha wananchi 99%, lakini nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kweli hatuna namna ya kukuelezea, lakini utasimuliwa kwenye historia ya nchi hii kwamba alikuwepo Waziri wa Maji Mheshimiwa Aweso na Makatibu Wakuu na Naibu wake Waziri pamoja na wakuu wa taasisi ambao wanakusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze *RUWASA*, nipongeze pamoja na wataalamu wote watendaji ngazi ya mkoa pamoja meneja wangu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunao Mradi wa Bujora ambao tenki kubwa limekamilika na hapa ndipo naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu tumepata shilingi bilioni tatu lile tenki lina *cubic litre* milioni tano na wameanza kutandaza mabomba kwenda sawa kwenye chanzo cha maji. Huu utakuwa ni mwarobaini kwa Mji wa Kisesa na Bujora ambao utanufaisha vijiji vya Kanyama, Bujora yenyewe, Wita, Igekemaja, Kitumba, Langi pamoja na pale Busekwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niombe sana kwamba sasa baada ya kukamilisha kupeleka bomba kwenye chanzo sasa mabomba ya kwenda kwa wananchi ambao hawana mradi wa uliopo sasa nayo yaendelee kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Kata ya Bujora pamoja na Kata ya Kisesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunao mradi wa Lutale - Langi ambao mwaka jana tuliuweka kwenye bajeti ya mwaka huu tunao malizia taarifa nilizonazo kutoka kwa Mkurugenzi wa *RUWASA* ni kwamba huu mradi utatangazwa mwisho mwezi wa sita. Kwa hiyo, niombe sana ni maradi ambao utanufaisha vijiji tisa tutamaliza matatizo ya wananchi kutoka Langi, Kageye, Itandula, Shilingwa, Sese, Ihushi, Matale, Igekemaja na vijiji vingine ambavyo vinazunguka karibu pale. Niombe pia mradi wa awamu ya pili Mradi wa Sola – Bubinza ambao kwa kweli ni mradi tumeanza kujenga chanzo kule Busega ambako kuna chanzo

kizuri tayari na tunategemea sasa lijengwe tenki kubwa pale Sola la *cubic litre* milioni mbili na ule mradi utanufaisha hata Tarafa nzima ya Ndagalu baada ya ukamilika napo nimetaarifiwa kutoka kwa Mkurugenzi wa *RUWASA* kwamba utatangazwa mwezi wa sita mwaka huu bajeti unayomalizia na kwenye bajeti hii umo umewekewa fedha kwa hiyo nikiombe sana taratibu hizi zote ziweze kukamilika nao utanufaisha vijiji 21 na mradi huu utakuwa ni mradi mkubwa sana ambao utasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe miradi ambayo inaendelea Mradi wa Iseni – Nyang'anga – Buhumbi; Mradi wa Misungwi – Kitongo; Mradi wa Sagani - Mwamabanza pamoja na Mradi wa Lugee -Kigambana, miradi hii ipo asilimia kubwa. Mradi wa Lugee - Kigangama ambao utanufaisha Kata ya Nyanguge na Mwamanga, mkandarasi amekwisha kufanya kazi zaidi ya shilingi bilioni tano, amelipwa shilingi bilioni moja, bado shilingi bilioni nne na amejenga tenki, amesambaza mabomba, bado kujenga chanzo, nimemwona hapa Naibu Waziri wa Fedha, niombe Wizara ya Fedha ipeleke fedha Wizara ya Maji ili iweze kulipa wakandarasi na wakandarasi waweze kuendelea ili watu waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Iseni - Nyang'anga nao uko asilimia 90, unategemewa kupewa tu fedha za kumalizia ili wananchi waweze kupata fedha na namna pekee ya kuweza kumtua mama ndoo kichwani ni hii, lakini Wizara hii kwa kweli imetoa fedha kwa ajili ya kuchimba visima, visima hivyo vimechimbwa kwenye vijiji mbalimbali, tumeyapandisha maji kwenye matenki, tumeanza kusambaza kwenye vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe Wizara hii kadiri ambavyo itaendelea kupata fedha tuweze kunufaisha wananchi kama ambavyo Wabunge wengi wameeleza kwamba sasa ni vijiji vichache ambavyo vimebaki havijafikiwa na maji. Tunaamini kwamba Serikali ya Awamu ya Sita ambayo imejipambanua kuhakikisha kwamba inawapatia wananchi maji tuone sasa kwenye hii bajeti, Mheshimiwa Aweso unapeleka fedha ili kuhakikisha kwamba fedha hizi zinanufaisha wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniventury.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniventura. Nilimtaja Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mheshimiwa Abdallah Jafar Chaurembo ajiandae.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi, awali ya yote na mimi niungane na Wabunge wenzangu wote ambao wamemshukuru Mheshimiwa Rais na mimi kwa niaba ya Wana-Kilwa, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu ameweka alama kubwa kwenye sekta hii ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na changamoto ya mradi wa miji 28 kwa miaka kumi sasa, lakini mwaka huu Mheshimiwa Rais amesema mradi wa maji miji 28 Kilwa utekelezeke na Wana-Kilwa wapate maji, shilingi bilioni 44 tumepata sisi wana Kilwa kwa ajili ya mradi ule kutoka Mavuji kwa ajili ya Miji ya Kilwa Kivinje na Kilwa Masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza mradi huu umekamilika maeneo yote, *treatment plant* tayari, tegeo tayari, minara miwili imeshajengwa kilichobaki ni usambazaji wa mabomba tunaomba msukumo wa Wizara ili mkandarasi aweze kusambaza mabomba maji yapatikane Kilwa Kivinje, Kilwa Masoko, Singino, Nangurukuru pamoja na vijiji vyote vinavyopitiwa na mtandao huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishukuru kwa mradi wa maji Kilwa Kisiwani, zaidi ya shilingi bilioni 1.6 zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya mradi huu na umesuasua kwa muda mrefu. Mheshimiwa Waziri, tunashukuru sana Wizara yako kwa heshima ambayo umetupa, umeleta msukumo mradi huu unatekelezeka, kilichobaki sasa hivi tunahitaji shilingi milioni 377 kwa ajili ya kwenda kusimika nguzo kupitisha maji baharini na bomba baharini ili Wana-Kilwa Kisiwani wakapate maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumenufaika na mradi ambao Wabunge wenzangu wote wamepata wa visima vitano vitano kila jimbo. Mimi nimepata katika Kijiji cha Makangaga, Rushungi, Kisongo, Mirumba pamoja na Mikoma. Ninavyozungumza ni kwamba Makangaga na Rushungi pamoja na Kisongo maji yameshapatikana, lakini Mirumba na Mikoma bado, tunaomba msukumo wa Wizara. Mheshimiwa Aweso, tunakusifia na tuna kuamini, hatukusifii kwa sababu tunapenda kukusifia, tunakusifia wewe na *Engineer* Kundo kwa sababu mnachapa kazi ambayo watanzania wanaiona. Tunaomba msukumo miradi hii ya visima vitano kila jimbo ikakamilike ili wananchi wetu wakapate maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na ule mradi wa mtambo wa maji katika mikoa yetu. Mimi katika Jimbo langu nilipata bahati ya kuchimbiwa baadhi ya visima katika vijiji kadhaa kikiwemo Kijiji cha Matandu, lakini maji hayajapatikana, Limaryao kule maji hayajapatikana. Mheshimiwa Aweso ninaamini kwa msukumo wako na nimeembiwa kwamba mtambo huu bado upo Kilwa, ninaomba mtambo huu usitoke Kilwa mpaka maji yapatikane katika vijiji nilivyovitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mradi wa kutoa maji Pande kupeleka Limaryao. Kata nzima ya Limaryao imekuwa na changamoto kubwa ya maji. Katika hili tulikuwa na *commitment* ya Shirika la Misaada la Kijerumani lakini tunaomba *intervention* ya Wizara katika hili ili tutoe maji Pande kupeleka Limaryao ambayo nimezungumza mara kadhaa hapa ni kata ambayo haijapata maji tangu izaliwe kwa maana ya maji yaliyo rasmi yanayopatikana katika utaratibu ule ambao umeratibiwa rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Wizara pamoja na watendaji wake wote wa Wizara, ikiwa ni pamoja na *Engineer* Mwajuma, Katibu Mkuu wetu, lakini pia Meneja wangu wa *RUWASA* wa Mkoa, lakini pia Meneja wangu wa Wilaya, ninaomba waongezewe nguvu. Kuna changamoto kubwa ya usafiri pale wilayani Kilwa, gari inayotumika ni mbovu, imechakaa ya muda mrefu ina kilomita zaidi ya laki nne. Kupitia bajeti hii

niombe Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa kuwasidia gari *RUWASA* Kilwa ili wakatekeleze miradi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho Wana-Kilwa tunaomba, ukatembelee miradi yetu hii, mradi wa miji 28 ukautembelee uone, mradi mkubwa wa kutoa maji Kilwa Masoko kupeleka Kilwa Kisiwani zaidi ya shilingi bilioni moja ukatembelee uone tunakualika sana na sisi tunasema tunakwenda na Mama Samia, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge. Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mheshimiwa Janejelly James Ntata ajiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nimshukuru Rais wetu Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu, lakini tatu nimshukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wanaoshughulika na sekta ya maji hasa viongozi wangu wa *DAWASA* pale Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Maji kupitia *DAWASA* katika Mkoa wa Dar es Salaam imefanya mambo makubwa sana. Kwanza nichukue nafasi hii kushukuru kwa miradi mikubwa ya upanuzi wa mtandao wa maji pale Dar es Salaam hasa katika Jimbo la Mbagala, zaidi ya shilingi milioni 389 zimetumika katika kuhakikisha miundombinu ya maji inawafikia wananchi na wananchi zaidi ya 200,000 wamenufaika na miradi ya maji katika maeneo ya Kimbangulile, Kizinga, Kijichi Mchikichini, Charambe, Makuka, Bamia, Msufini, Rufu, Moringe, Mji Mpya, Machinjioni A, Kokoto, Goroka, Kiponza, Rangi Tatu, Bugudadi na maeneo ya Nyambwela.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyataja maeneo haya kwa sababu ni watu ambao muda mrefu walikuwa hawapati huduma nzuri ya maji, lakini sasa hivi kwa kupanuliwa mtandao wa maji wameanza kupata maji na kwa kweli na wao wanaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niishukuru sana Serikali kwa miradi mikubwa miwili ambayo inaendelea, mradi ule wa kutoa maji Mto Rufiji. Mradi ule utakapokamilika, naamini katika Jimbo langu la Mbagala matatizo ya maji yatakuwa ni historia lakini kuna ule mradi wa Bwawa la Kidunda ambalo ninamini linaenda kuongeza nguvu katika upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niendelee kuwapongeza na kushukuru huduma ya usafi na mazingira, katika Jimbo langu la Mbagala tumepata vyoo vya umma vinne ambavyo vimejengwa katika maeneo ya soko la Rangi Tatu, Mbande, Kampochea na maeneo ya Toangoma. Kwa kweli, Wizara pamoja na *DAWASA* kwa ujumla wamefanya kazi kubwa sana katika Jimbo langu la Mbagala lakini bado tunayo changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, alitembelea pale Charambe, ameona lipo eneo halina mtandao kabisa wa maji ya *DAWASA*. Tunayo maeneo ambayo yana matatizo, maeneo ya Maji Matitu, maeneo ya Chasimba, maeneo ya Kilungule, maeneo ya Machinjioni B na Machinjioni C, maeneo ya Dovya, maeneo ya Kisewe na baadhi ya maeneo ambayo kwa kweli bado yamekuwa na changamoto ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukuombe sana ili Dar es Salaam ikamilike, wakazi wengi wa Dar es Salaam wanapatikana katika maeneo haya. Tukuombe sana katika hiki kipindi kilichobaki yapo mambo tunaweza tukayafanya maeneo haya yakapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; tunacho kisima pale panapoitwa Mabomba Nane, eneo lile kile kisima kina maji mengi, maji yale tukiyaongezea *booster pump* yanaweza yakapeleka Kilungule, Chasimba na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya yamekuwa na matatizo ya maji, si kana kwamba hakuna visima, lakini maji yanayopatikana ni ya chumvi, hayafai katika matumizi ya binadamu. Pia eneo la Dovya ipo chemchem kubwa ya maji imeonekana pale. Tuwaombe sana, sisi Dar es Salaam

tunafahamu hatujapata magari ya kuchimbia visima vya maji, lakini tuombe yatafutwe mazingira yoyote maeneo haya yaende yakachimbwe visima vya maji, kwa sababu vyanzo vya maji vimeonekana na bahati nzuri *DAWASA* wamepima wameona maji yale yanafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, *DAWASA* wana *water bowser,* naomba *water bowser* zile zitumike vizuri ku-*supply* maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Chaurembo. Tunaendelea na Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTANTE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, nami nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa uweza. Niungane na wote waliokupongeza Waziri wa Maji Jumaa Aweso, libarikiwe tumbo lililo kuzaa na niwaombe Wana-Pangani wasifanye makosa, wakurejeshe na jicho la Mheshimiwa Rais likuone umalizie kazi uliyoianza, lakini nikupongeze Naibu Waziri, mimi huwa nakuita simba mwenda pole, lakini mkali kama pilipili wakichezea miradi ya maji, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Bi. Mwajuma ambaye ni mtaalamu mbobezi wa maji mtiifu na mnyenyekevu tofauti na kazi anazozisimamia, lakini mna Naibu Katibu Mkuu ambaye ndiyo mtaalamu wa uchambuzi wa sera, Bi. Agnes Meena, yawezekana ndiyo imesababisha hata sera ya maji sasa mmeibadilisha, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha anataka kumtua mwanamke ndoo kichwani, pale alipoamua kuongeza bajeti kutoka shilingi bilioni 680 hadi shilingi trilioni moja, si kazi ndogo na kwenye hiyo bajeti lipo Bwawa la

Kidunda, Bwawa la Kidunda ni mwiba unaoenda kumaliza shida ya maji Pwani, Morogoro na Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefanya kazi maji, nilianza kazi nikakuta Bwawa la Kidunda, leo niko Bungeni nimeongelea Bwawa la Kidunda nikiwa kwenye Kamati, lakini Mama Samia ameweza kuvunja kitendawili kile na kukitegua sasa Kidunda inaenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri hapa kwenye Kidunda, Kidunda kwa Morogoro itaenda kumaliza mgogoro wa wakulima na wafugaji kama mkishirikiana na Wizara ya Mifugo kwa kuweka sehemu za unyweshaji ili mifugo sasa ipate mahali pa kunywa maji iache kupita kwenye mashimba ya wakulima, lakini mkiwasiliana na uvuvi mkapanda vifaranga tunaenda kumaliza *shortage* ya Samaki, lakini kwa ukame wa Dar es Salaam na Mto Ruvu kukosa maji Kidunda inaweza kumaliza hilo tatizo, niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze kwa namna mlivyokiendeleza Chuo cha Maji kutoka kwenye udahili wa wanafunzi 2,320 hadi 4,260 sawasawa na 84% si jambo dogo, lakini mmeanzisha *consultancy bureau* ambayo mmeamua kuwakumbuka wastaafu, kwa hili nikupongeze na Wizara zingine igeni, kustaafu kwa miaka 60 siyo kwamba akili imezeeka, ng’ombe hazeeki maini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkiwatumia hawa wastaafu, Mheshimiwa Aweso upo kwenye kundi la maji huwa unaona utaalamu unaotiririka pale kutoka kwa wataalamu walio staafu wa maji yawezekana hapo ndipo ulipompata hata *CEO*. Sasa Bwire uliyokuwa unatiririsha pale ukayafanye *DAWASA*. Wapo wataalamu wamebobea nani kushukuru jana nimeona umealika hata wastaafu, ni kazi nzuri sana Wizara zingine igeni, hawa wastaafu tukiwatumia, nchi itafika mahali ambapo ni pazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze kwa kujenga Mradi wa Banguro, mnaenda kumtua mwanamke ndoo kichwani,

wanawake wa *Pugu station*, wanawake wa Gongo la Mboto, Kivule, Kata zote za Ukonga, lakini unapeleka maji mpaka Kibamba, hii ni kazi kubwa sana mmefanya na mmeamua kutumia shilingi bilioni 36.8 kuhudumia wananchi 250 siyo kazi ndogo na pesa zimetiririka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nishauri, siasa za Dar es Salaam ni maji, niombe muendelee kutumia visima vya Kisarawe II vikasambaze maji maeneo ya Kariakoo, maeneo ya Mbagala na maeneo mengine ambayo yana ya shida ya maji kwa sababu mwanamke wa Dar es Salaam hatuombi ruzuku ya mbolea, hatuombi ruzuku ya pembejeo, sisi tunachoomba ni maji. Siasa ya Dar es Salaam ni maji, kura za Dar es Salaam zinapatikana kutokana na maji. Niombe muangalie upatikanaji wa maji wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmenunua vifaa vya maji taka, Dar es Salaam shida yetu ni maji taka, hebu *DAWASA* waongeze *speed* ya kutoa maji taka kwenye mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga hoja mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Janejelly James Ntate. Nilimtaja Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mheshimiwa Aysharose Mattembe ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, na mimi nimshukuru *Allah Subhanahu Wa Ta'ala* kwa kutujalia uzima, uhai lakini halikadhalika, niwapongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, lakini na timu nzima ya watendaji wa Wizara ya Maji ikiongozwa na *Engineer* Mwajuma, kwa kweli kwa utendaji wao uliyotukuka. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maji nimeweza kuwa nao karibu na nimeona jinsi Mheshimiwa Waziri alivyotengeneza timu bora ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mwenyekiti wangu wa Kamati, kwa kweli kila mkoa unaokwenda unahisi kama kuna *photocopy* imechukuliwa halafu imekwenda kuwa-*pasted* sehemu fulani. Watendaji wanafanana nidhamu, wanafanana ubora na wanafanana uwezo. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri na timu yako hongera kwa kutengeneza ufanisi mzuri katika Wizara ya Maji na ndiyo maana hakuna mtu ambaye atashangaa kuyaona mafanikio haya ambayo wajumbe hapa wa Bunge hili Tukufu wameweza kuyazungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa kweli amechagua majembe, amechagua jembe Mheshimiwa Waziri, amechagua jembe Mheshimiwa Naibu Waziri, amechagua jembe Jemedari wetu *Engineer* Mwajuma, kwa kweli hii ni mihimili na Mwenyezi Mungu aiweke kwa sababu matumaini makubwa kwamba hawa ndiyo wataondosha changamoto ya maji kupitia Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini halikadhalika Mheshimiwa Waziri unafanya kazi nzuri na una jicho kwa sababu kila unayemteua ana sadifu, kwa sababu nikiangalia juzi tu umechagua Mtendaji Mkuu wa *RUWASA* kwa kweli anafanya kazi nzuri, tumeshuhudia. Tumekwenda kule Manyara tumeona kazi yake nzuri aliyoifanya, sisi tulimuona, lakini nashangaa na wewe ukamuona ukamsogeza karibu afanye kazi kwa uzuri zaidi. Kwa hiyo, hongera sana na yeye tunamwombea heri azidi kuleta mabadiliko katika *RUWASA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka minne katika Bunge lako hili Tukufu kwa kweli kipindi cha Mama Samia kimeshuhudia *reforms* nyingi za maji. Tumeona hapa, wenzangu wamezungumza, sera ya maji ambayo ilikuwa ina zaidi ya miaka kumi naa huko hivi sasa imebadilishwa imefanyiwa marekebisho na imeridhiwa na tuna toleo jipya la mwaka 2025, na lenyewe sera zaidi inaelekeza kwanza kuweza kuratibu vizuri, lakini vilevile kujumuisha taasisi mbalimbali na Wizara ziweze kufanya kazi kwa pamoja, pamoja na kuwajumuisha wenzetu wa *private sectors* ushiriki wao katika huduma za kuendeleza masuala ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetumia nafasi hii kuwaomba wadau wa maendeleo wakiwemo *private sectors* tusaidie Wizara ya Maji kwa sababu huku ni ucha Mungu, lakini halikadhalika ni kusaidia jitihada za nchi kuweza kuendeleza harakati za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pamoja na mafanikio makubwa ambayo yamekuja kwenye hii Wizara, mimi nina ushauri wa mambo mawili makubwa, haraka haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa kwanza, tunajua mama ameonesha utashi mkubwa kuongeza bajeti kutoka shilingi bilioni 680 hadi shilingi trilioni moja katika kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha. Sasa fedha hizi kama tutakwenda kutumia zote kulipa madeni, tutabakiwa na fedha kidogo sana kuweza kuendeleza huduma za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba sana tumuombe Waziri wa fedha afanye kila linalowezekana fedha za madeni zile shilingi bilioni 500 azitafute sehemu nyingine na hizi shilingi trilioni moja zikafanye kazi ya kwenda kuelekeza huduma za maji moja kwa moja ikiwemo miradi mipya kwa sababu kama tutatumia fedha hizi kwa viporo vya miradi basi fedha hizi hazitatosha kuendeleza miradi mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika nimpongeze Mheshimiwa Waziri ametengeneza huu Mfuko wa Maji katika hali nzuri zaidi hivi sasa na Mtendaji yule kijana Haji anafanya kazi vizuri. Sasa ningeomba tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha akajitahidi fedha za makusanyo zinazopitia mfuko wa fedha yaani kwa huduma za maji zote zipelekwe kwenye Mfuko wa Maji bila kuwapatia asilimia fulani kwa sababu tukizi-*portion* kidogo basi tunapunguza ule umadhubuti wa kwenda kufanya kazi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huu mchakato wa *accreditation* kwa ajili ya *GCF*. Mheshimiwa Waziri hongera umeanza mchakato huu, lakini ningeomba tu vijana wako ni mahiri huu kuuendeleza mwa haraka kwa sababu taasisi karibu tatu ambazo zipo TAMISEMI, Wizara ya Fedha pamoja na wenzetu

wa *NEMC* wameshaanza huu mchakato, lakini sasa hivi ni mwaka wa kumi bado hatujafanikiwa kuweza kupata *accreditation* au usajili kwa ajili ya Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi wa *GCF*. Nategemea kwamba wewe utakuwa ni mdau wa kwanza katika Taasisi za Serikali ukiondosha Benki ya CRDB kuweza kwenda kuwa mdau wa *GCF Insha'Allah. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah. Nilimtaja Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mheshimiwa Tecla Ungele, ajiandae.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia uzima na afya njema na ameniwezesha kusimama hapa siku hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara namba moja wa kampeni ya kumtua mama ndoo kichwani na hii imejihirisha kwa namna ambavyo amenunua mitambo 25 ya kuchimbia visima nchini kote na katika Mkoa wangu wa Singida. Mheshimiwa Rais tunakushukuru na tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Waziri kaka yangu Mheshimiwa Aweso kwa kweli unafanya kazi nzuri sana wewe pamoja na Naibu Waziri kama yangu *Engineer* Kundo na timu nzima ya Wizara ya Maji mnafanya kazi nzuri sana, ninawapongezeni wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mimi leo hapa nasimama kutoa shukrani zangu nyingi kwa namna ambavyo tumepokea fedha nyingi za kutekeleza miradi ya maji katika Mkoa wangu wa Singida. Katika mwaka huu wa fedha tumepokea shilingi bilioni 16 na miradi 43 imeweza kutekelezwa katika Mkoa wangu wa Singida. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt.

Samia Suluhu Hassan ambaye amemtua ndoo Mwanamke wa Singida. Kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Singida ninasema ahsante sana na tunakushukuru Mheshimiwa Rais tuko pamoja na wewe bega kwa bega kuhakikisha kwamba ifikapo Oktoba, 2025 unapata kura zote za ndiyo katika Mkoa wangu wa Singida. Mheshimiwa Rais tunakushukuru na tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kushukuru kwa Mradi wa Maji Kintinku - Lusilile. Mradi huu wa maji ulikuwa ukisuasua kwa muda mrefu sana, lakini kwa sasa mradi huu umekamilika na Wananchi wa Wilaya ya Manyoni wanakunywa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Wilaya ya Manyoni wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwatua ndoo kichwani kwa sababu ukanda wote wa miji ya Kintinku na Lusilile ulikuwa una changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama na maji yake ukichimba chini unakutana na chumvi, hayafai kwa matumizi ya binadamu lakini sasa mradi huo umekamilika, tunashukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru miradi ya miji 28 ambapo katika Mkoa wangu wa Singida miradi hii inatekelezwa katika mji wa Kiomboi, Manyoni na Singida. Niombe sana mchakato wake uendelee kwa haraka kwa sababu miji hii ina uhaba mkubwa wa maji na imekuwa kwa kasi ukilinganisha na mahitaji yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishukuru sana kwa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria. Mradi huu umeshafika katika Tarafa ya Shelui, Wilaya ya Iramba, lakini vipo vijiji ambavyo viliwekwa katika mpango na vijiji hivyo havina maji mpaka sasa hivi. Vijiji hivyo ni Mgongo, Mtoa, Mgela, Kibirigi, Mseko na Msai. Niombe sana kwa kuwa mchakato unaendelea na vijiji hivi viweze kupatiwa maji ya Ziwa Victoria, lakini kwa kuwa pia mradi huu wa maji wa Ziwa Victoria unapita katika Mkoa wangu wa Singida na usanifu unaendelea, niombe sana vijiji vyote, kata na wilaya maji haya yapite. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Katika Mkoa wangu wa Singida kuna changamoto kubwa sana ya

upatikanaji wa maji safi na salama na unategemea vyanzo vya visima. Sasa njia pekee ya kumkomboa mwanamke wa Mkoa wa Singida ni maji ya Ziwa Victoria na tumewaambia kwamba yatapita maji haya kwa kilometa 12 pale mradi unapopita. Kwa hiyo, niombe maji haya yapite katika maeneo yote ya Mkoa wa Singida kwani ndiyo mwarobaini pekee wa kuweza kumkomboa mwanamke wa Singida kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishukuru katika Wilaya yangu ya Mkalama tumepata maji katika Vijiji vya Malaja, Nkalakala, Mwangeza na Mbigigi, lakini pia yako maeneo katika Wilaya ya Mkalama ambayo yana changamoto kubwa sana ningeomba yaangaliwe kwa kina. Maeneo haya ni Mwangeza, Singa, Mpambala na Kijiji cha Nyahaa, lakini pia kwa Wilaya ya Ikungi pia tumepata maji ipo changamoto kubwa katika Wilaya yangu ya Ikungi, Mji wa Ikungi pale kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa sababu mji huo tayari umeshakua. Niombe sana Mheshimiwa Waziri uangalie kwa kina jambo hili ili wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naomba dakika moja, kwa kumalizia ipo changamoto kubwa ya upatikanaji wa vitendea kazi hasa katika Wilaya ya Ikungi, Manyoni na Singida niombe katika wilaya hizi kwani jiografia yake ni ngumu sana. Nakushukuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Aysharose. Nilimtaja Mheshimiwa Tecla Ungele, Mheshimiwa Innocent Bilakwate, ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uzima, lakini nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi kubwa za kuwapatia Watanzania maji safi na salama. Tunaona miradi kote nchini inaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Aweso na Naibu wake *Engineer* Kundo. Waziri Aweso huyu anatekeleza yale maono ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani. Ninampongeza sana, ni kijana mwenye juhudi kubwa muda wake mwingi anautumia kwa kazi hakika Mwenyezi Mungu ambariki sana. Pia nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Maji na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia hata mameneja kwenye mikoa. Mkoa wa Lindi - *Engineer* Lubasa na Ma-*engineer* wake wale mameneja wa wilaya zote za Mkoa wa Lindi wanafanya kazi kubwa ya kutekeleza miradi na usimamizi mkubwa wa miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mingi, lakini baadhi tu ya miradi mimi ni Mbunge wa Mkoa mzima wa Lindi, lakini nasema miradi mikubwa ya miji 28, mradi ule wa Mavuji kupeleka maji Nangurukuru, Masoko na Kivunje shilingi bilioni 44 umeshakuwa na tenki tayari pale Singino lakini bado sasa kusambaza mabomba tu kupeleka Kivinje na kule Nangurukuru na pia tenki lingine la kupeleka maji kule Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna Mradi wa Nyangao kupeleka maji Ruangwa na vijiji 21 za Wilaya ya Nachingwea ni kazi kubwa inafanyika kwa Wizara hii. Mheshimiwa Waziri sisi Wana-Lindi tunakushukuruni sana kwa kazi yenu mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashukuru kwa Wilaya ya Nachingwea kupeleka maji kule Kata ya Ngunichile. Wana-Ngunichile wameishi kwa maji ya kuokotaokota tangu misingi ya dunia hii iwekwe, lakini sasa hivi wanaenda kupata maji safi na salama. Tunawashukuruni sana Wizara, tunamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, haya mambo hatujawahi kuyaona ndiyo uongozi huu wa Dkt. Samia Suluhu Hassan lakini hata pia wa Mchinga wanapata maji safi na salama sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo kadhaa, tunaposhukuru namna hii Mheshimiwa Waziri, lakini pia

tunavyoshukuru hatuachi kuomba tena. Kuna changamoto kubwa, naona ukurasa wa 29 wa hotuba yako Mheshimiwa Waziri umesema kwamba kuna uchunguzi unaendelea ufuatiliaji wa maji ya matumizi ya majumbani. Tumeona Mkoa wa Lindi na Mtwara kumeonekana maji yake yana madini ya chumvi, chuma na *manganese*. Sasa ndiyo maana sisi Wanalindi tunaomba ule mradi wa kutoa maji kutoka Rufiji kuleta Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rufiji siyo mbali kutoka Rufiji kuja Kilwa, halafu unakuja Lindi na ukitoka Mto Ruvuma unakuja pale Mangaka halafu unavuka tu unakuja Wilaya ya Nachingwea unaenda Wilaya ya Ruangwa. Kwa hiyo, maji yale yatakuwa maji salama lakini maji ya uhakika kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwa uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama kwingine kunafanyika miradi mikubwa kutoa maji kwenye maziwa makuu kupeleka sehemu mbalimbali nchini Tanzania atashindwa kweli kutoka Rufiji kuleta hapo Lindi? Kutoka Ruvuma kuleta Lindi Nachingwea na Liwale? Nafikiri jambo hili kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni rahisi sana na ndiyo maana ameongeza bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna wale watendaji wetu wa Mkoa wa Lindi wana magari machakavu, hayawezi hata kwenda huko mbali tunakofikiria. Magari ni machakavu, Mheshimiwa Waziri mimi ninaomba utakapopata bajeti yako na kufanya mkakati wa kununua magari, basi naomba uwapelekee watendaji wetu wa Idara hii ya Maji kule Mkoa wa Lindi ili wafanye kazi ya ufuatiliaji na usimamizi wa miradi hii mizuri kwa wakati muafaka. Fikiri mtu yuko Kilwa – Masoko, *Engineer* Sultan yuko pale Kilwa Masoko anataka afuatilie mradi kule Kandawale zaidi ya kilometa 100, unafikiri anafikaje na gari chakavu namna ile. Hebu fikiria *Engineer* Musiba yupo pale Nachingwea anafuatilia mradi wa maji kule Kiegei au Kilimarondo zaidi ya kilometa 100 anafikaje na mle njiani kuna wanyama wale wakali, tembo. Ni hatari sana, chonde chonde tunaomba magari utakapo magari mapya basi naomba uwakumbuke maengineer wetu wa Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipatia na nampongeza Mheshimiwa Rais, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tecla Ungele. Nilimtaja Mheshimiwa Innocent Bilakwate Mheshimiwa Zaytun Swai, ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia kuendelea kuwepo katika Bunge hili kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha anamtua ndoo mama kichwani. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu yako kwa ushirikiano mkubwa ambao mmekuwa mkinipa ninapokuja ofisini kufuatilia miradi ya maji kwa ajili ya Wilaya ya Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze *RM* wa Mkoa wa Kagera kwa kazi nzuri na ushirikiano anaotupa sisi Wabunge bila kumsahau kijana wetu Kashonele anayekaimu pale Wilaya ya Kyerwa, kwa kweli anafanya kazi nzuri na niombe sana Mheshimiwa Waziri ikikupendeza kijana huyu amekaimu zaidi sasa hivi ya miezi sita ikiwezekana mpe kabisa nafasi hii kwa sababu anaweza kazi, ninaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa miradi ambayo umetupa Kyerwa tunakwenda vizuri, lakini miradi hii imekuwa na madeni mengi. Mmejitahidi kuwa mnatulipa kidogo, lakini wanadai hela nyingi sana. Wakandarasi hawa hizi hela wanakopa kutoka benki na wanapokopa hizi hela kutoka benki, benki haiangalii Serikali imelipa au haijalipa, wanaendelea kulipa riba na mwisho wa siku hawa wakandarasi tusipowaangalia wanaenda kufilisiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, tuombe sana Waziri wa Fedha wakandarasi hawa waweze kulipwa ili wakamilishe hii miradi. Kwa mfano nina Mkandarasi huyu Otonde amefanya mradi pale Kikukuru wa zaidi ya shilingi bilioni tano mpaka sasa hivi mradi umefika 75% anadai zaidi ya shilingi bilioni 3.1; kuna huyu Jamta mradi wa Lunyinya - Chanya anadai shilingi bilioni 2.2; Mradi wa Kaisho Isingiro anadai shilingi milioni 420, kuna huyu Amri Karim anadai shilingi milioni 200. Miradi hii iko kwenye hatua nzuri na bila Mheshimiwa Waziri kuwalipa hawawezi wakakamilisha miradi hii, wametoka *site* wananchi wanasubiria maji na unajua kipindi hiki wale wanaotafuta Ubunge wanasema ni miradi hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri Wana-Kyerwa wanahitaji maji hawahitaji kuona mabomba tu yametandazwa wanachohitaji ni maji. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, ninajua wewe ni kijana mpambanaji hebu pambania hii miradi iweze kukamilika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Waziri niliomba visima vya maji mkanipatia visima vya maji ambavyo tumechimba kwenye Kata ya Nyakatuntu, Nyaruzungura, Kamuli, Nyakakoni, Songambele na Omuchwekano. Naomba sana miradi hii ikamilike, wamechimba lakini kwa kweli kasi inayoendelea siyo nzuri na unajua tunao ule mradi mkubwa na tuliomba hivi visima wakati tunasubiria mradi mkubwa. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa wazirimiradi hii ikamilishwe. *(Makofi)*

Kwa hiyo nakuomba sana Mheshimiwa Waziri tunajua unachapa kazi nzuri sana hatuna mashaka na wewe kwa hiyo niombe sana miradi hii iweze kukamilishwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilisemee hizi fedha za tozo ambazo tumepitisha sisi kama Bunge; fedha hizi zimekuwa zikiletwa kidogo, lakini zinakuja kwa kuchelewa, fedha hizi tumezipitisha sisi Wabunge, niombe sana kama kuna uwezekano tupitishe azimio, fedha hizi ziwe zinakuja moja kwa moja kwenye Wizara ya Maji kwa sababu tumeshazipitisha tunatamani tuone miradi hii inakamilika wakati mwingine fedha

zinakuja zimechelewa, watu tunaweza tukaanza kumlaumu Mheshimiwa Aweso, lakini mimi ninajua kwa jianzi ambavyo amejipanga Mheshimiwa Aweso anatamani kuona miradi hii inakamilika sasa bila kumpatia fedha miradi hii haiwezi kukamilika. *(Makofi)*

Kwa hiyo niombe sana Bunge hili tulijadili na ikiwezekana tupitishe azimio miradi hii iweze kupewa hela na iweze kukamilika na Watanzania waweze kufurahia matunda ya Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa

Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wa Maji, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Maji, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi kumi ya bajeti ya 2022/2023, Serikali kupitia Wizara ya Maji imetekeleza miradi mingi ya maji. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya inatekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi ya vijiji vya Simambwe, Usoha Njiapanda, Tembela, Iyawaya, Izyira, Ruanda, Ilembo, Inyala, Igoma, Iwalanje, Galijembe, Tembela, Pashungu, Shigamba, Santilya, Inyala Ilembo, Mshewe, Muvwa, Njelenje, Mapogoro, Mjele, Chang'ombe, Ipwizi, Ikukwa, Simboya, Itimba, Utengule, Ihombe, Idugumbi, Iwala, Ilota, Ikhoho na pia mradi mkubwa katika Mji Mdogo wa Mbalizi. Miradi yote hiyo

imetekelezwa kwa ufanisi mkubwa, ingawa kunahitajika uboreshaji wa miundombinu ya mabomba hasa katika mradi wa Mbalizi kuna upotevu mkubwa wa maji kutokana na uchakavu wa mabomba yaliyokuwepo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo makubwa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya bado kuna changamoto kubwa ya maji salama kwa wananchi. Pamoja na kuwepo kwa vyanzo vingi vya mserereko *(gravity),* asilimia kubwa ya vijiji havina maji salama. Nashukuru kwa kuwepo bajeti ya mradi mkubwa wa Mto Kiwira ambao utakuwa mkombozi wa maeneo mengi ya Mkoa wa Mbeya na hata Songwe. Napendekeza Serikali iendelee kutekeleza miradi ya maji kwa mpango wa *force account* ambao umeonesha mafanikio ya kupunguza gharama za miradi na pia utekezaji ni wa haraka na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali iweke msukumo mkubwa wa kuharakisha utekelezaji wa miradi iliyomo kwenye Mradi wa Bonde la Mto Songwe *(Songwe River Basin Development Programme - SRBDP),* wenye ofisi zake Kyela, Tanzania. Mradi huu unaotekelezwa kwa pamoja na Serikali za Tanzania na Malawi, ni muhimu sana kwa sasa kutokana hasa na ujenzi wa mabwawa ambayo pamoja na manufaa mengine, yatasaidia kupunguza mafuriko ya Bonde la Kyela. Mabwawa haya yamelenga kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji, shughuli za uvuvi na hata utalii ambao unahitajika sana katika Wilaya ya Mbeya na ukanda wote wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto za tabianchi, kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa mazingira na ongezeko la upungufu wa vyanzo vya maji. Uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu umepelekea misitu mingi kuharibiwa na uchomaji moto, ukataji mkaa na hata kilimo kwenye vyanzo vya maji. Napendekeza Serikali iongeze msukumo wa Wizara za Maji, Kilimo, Maliasili na Mazingira kufanya kazi kama timu moja ili kukabiliana na janga hili kubwa ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko. Kama ilivyo kwa athari za mafuriko ya Kyela, hata Ziwa Rukwa

linaathirika sana na kujaa mchanga na udongo unaosombwa na mito kutokana na mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mahitaji ya maji kwenye kilimo, mifugo na hata mahitaji ya mabwawa kwa ajili ya kuzuia mafuriko ikiwemo kwenye miundombinu yetu ya reli na barabara, kuna haja na kuwepo kwa taasisi moja kuratibu na kusimamia mipango ya matumizi ya maji. Nchi yetu ina neema kubwa ya maji na hii ni fursa ya kipekee kutumia haya maji kama mojawapo ya nguzo kuu kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Maji Mheshimiwa Jumaa Aweso (Mb.) na Naibu wake Mhandisi Mathew Kundo (Mb.), Katibu Mkuu Mhandisi Mwajuma Waziri, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Agnes Kisaka Meena na wataalamu wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri wanayofanya. Kwa namna ya pekee niwashukuru sana watendaji wa Wizara ya Maji waliopo mkoani Kilimanjaro ambao ni Wahandisi Kija Limbe *(MUWASA),* Weransari Munis *(RUWASA* Mkoa) na Musa Msangi *(RUWASA* Wilaya) kwa ushirikiano wao mkubwa na Mbunge kuwapatia wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri na timu yake wamekuwa mfano wa kuigwa kwenye kutatua changamoto za maji na kuwatua akina mama ndoo kichwani, kwani maji ni haki ya msingi kwa binadamu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, inatia faraja kuona upatikanaji wa maji vijijini unaongezeka kutoka 70.1% mwaka wa 2020 na kufikia 83% mwezi Disemba, 2024. Kwa upande wa mjini, upatikanaji wa maji unaongezeka kutoka 84% mwaka wa 2020 na kufikia 91.6% mwezi Disemba mwaka 2024 kama alivyoonesha kwa kina katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka huu wa 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji hapa nchini kutokana na uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu na pia nitaongelea changamoto za maji katika jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina utajiri mkubwa wa vyanzo vya maji. Tunayo mito mikubwa na midogo, maziwa na kiasi kikubwa cha maji chini ya ardhi. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira, kuna hatari kubwa ya kuja kukabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi hapa nchini yanakabiliwa na uharibifu wa vyanzo vya maji kutokana na shughuli za binaadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa hatua walizochukua kubaini vyanzo vya maji hapa nchini. Ripoti ya Waziri imeonesha kwamba hapa nchini kuna idadi ya vyanzo 3340 ambapo vyanzo 350 vimewekewa mipaka na vyanzo 68 vimetangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu. Kwa ujumla, maeneo ambayo Serikali haijaweka mipaka, kuna uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwani kwenye vipaumbele vya mwaka 2025/2026, uhifadhi na uendelezaji wa vyanzo vya maji umepewa nafasi kubwa kwenye utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii ya uharibifu wa mazingira katika vyanzo inaweza kusababisha maji kupungua na mara nyingine kuchafuka, hali inayohatarisha afya za watumiaji, jambo linaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Waziri amekiri kwamba bila maji, hakuna Taifa. Hivyo basi ni vyema kulinda vyanzo hivi vya maji kwa manufaa ya usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hii hatarishi ya uharibifu wa vyanzo vya maji, ninaishauri Serikali ichukue hatua kali zifuatazo:-

Mosi, Serikali kupitia kwa Mamlaka za Maji na *RUWASA* watoe elimu kwa wananchi katika maeneo husika kuhusu faida za kutunza vyanzo vya maji. Elimu hii itolewe kuanzia ngazi ya vitongoji na vijiji. Ninaishauri Serikali itenge bajeti ya kutosha ili kuwawezesha watoa elimu kwa umma kuwafikia wananchi walio karibu na maeneo ya vyanzo vya maji. Wahusika watoe elimu pana juu ya athari za uharibifu wa vyanzo vya maji na namna ya kuvitunza, ikiwa ni pamoja na kuwapatia miti rafiki na kuipanda kwenye maeneo ya vyanzo vya maji.

Pili, kwenye maeneo yanayoendesha shughuli za kilimo na ufugaji, Serikali itenge maeneo maalumu ya kulima na kufuga na iwe ni marufuku kabisa kufanya shughuli zozote za kibinadamu (kilimo na ufugaji) katika vyanzo vya maji. Mifugo itafutiwe sehemu maalumu ya kunyweshwa maji na isionekane kabisa kwenye vyanzo vya maji. Kwa kulitekeleza hili, hakutakuwa na athari za uharibifu na uchafuzi wa vyanzo vya maji.

Tatu, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ziimarishe sheria zote kuanzia ngazi ya Taifa hadi vijijini zitakazolenga kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sheria kali zitawekwa kuanzia ngazi ya kijiji zitakazohusu udhibiti na uhifadhi wa maeneo ya vyanzo vya maji, basi itasaidia kwa kiasi kikubwa kukabiliana na janga hili ambalo kila siku Serikali imekuwa ikitoa matamko, lakini ufuatiliaji wa sheria juu ya watu wanaohatarisha vyanzo vya maji unakua mdogo. Ni muhimu utekelezaji wa sheria hizi ufuatiliwe na adhabu zilizowekwa zitekelezwe kama ilivyoainishwa kwenye sheria.

Nne, katika Idara ya Maliasili, Serikali imeweka vifaa/teknolojia maalumu kudhibiti maharamia wanaowinda na kuua tembo. Ni vyema Serikali ikaanza programu ya kuweka vifaa vya kisasa ambavyo vitasaidia kuoanisha maeneo yote yenye

vyanzo vya maji nchini, ili kuonesha uharibifu wowote utakaofanyika kutokana na shuguli za binadamu. Jambo hili likifanikiwa itasaidia sana kulinda na kuokoa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu la Moshi Vijijini, kuna changamoto ya upatikanaji wa maji ya bomba katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali kwa kutoa shilingi 486,192,492.42 na kutekeleza mradi wa kupeleka majisafi na salama katika Kata ya Mbokomu. Pesa hizi zimetumika kufanya uboreshaji na upanuzi wa mtandao wa majisafi urefu wa kilometa 24.7 katika Vijiji vya Korini Juu, Korini Kati na Korini Kusini. Katika mradi huu, jumla ya bomba zenye urefu wa kilometa 11.6 kati ya 24.7 sawa na 47% zimekamilika. Baadhi ya wananchi wameanza kunufaika na mradi kwa kupata majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado 53% ya mabomba yanahitajika na kuna uhitaji wa fedha kiasi cha shilingi 357,682,020.98 ili kukamilisha kazi zilizopangwa na *MUWASA* ambazo zinalenga kusogeza mtandao wa bomba karibu zaidi na wananchi na kuwapunguzia gharama za maunganisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kimochi ina zaidi ya wakazi 16,046. Kata hii ina Vijiji vya Mowo, Sango, Shia, Miami, Lyakombila na Kisaseni. Eneo lote linahudumiwa na *MUWASA* Tunaishukuru Serikali kwa kutoa shilingi 983,668,163.13 kujenga mradi wa majisafi na salama katika Kata ya Kimochi. Kazi zilizofanyika ni za upanuzi wa mtandao wa majisafi urefu wa kilometa 44.3 katika Vijiji vya Sango, Shia, Kisaseni, Mowo Lyakombila na Mdawi. Katika mradi huu, jumla ya bomba zenye urefu wa kilometa 26.5 kati ya 44.3, sawa na 59.8% zimekamilika kwa kutumia fedha kutoka Wizara ya Maji. Aidha, chanzo cha maji Muo kimejengwa kwa kutumia mapato ya ndani na wananchi wanaendelea kupata maji kutoka katika mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Kimochi, bado kuna uhitaji wa fedha kiasi cha shilingi 483,668,163.13 ili kukamilisha kazi

zilizopangwa zinazolenga kusogeza mtandao wa bomba karibu zaidi na wananchi na kuwapunguzia gharama za maunganisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mabogini ina wakazi wengi (57,231) na bado kuna changamoto ya maji ya kunywa katika baadhi ya maeneo. Tunaishukuru Serikali kwa kutoa shilingi 2,184,373,327.5 kutekeleza miradi ya kupeleka majisafi na salama katika Kata ya Mabogini. Kazi zilizofanyika ni upanuzi wa mtandao wa majisafi urefu wa kilometa 55.45 katika Vijiji vya Mji Mpya, Mvuleni, Maendeleo, Mtakuja, Chekereni, Muungano na Mserekia. Mradi umekamilika kwa 100%. Sasa hivi wananchi wanapata huduma ya majisafi kwa saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama takwimu za sensa zinavyoonesha, eneo hili linakuwa kwa kasi, hivyo kinahitajika kiasi cha shilingi 175,000,000 kwa ajili ya upanuzi wa mtandao wa bomba urefu wa kilometa 12 ili kupunguza gharama za maunganisho kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa uwekezaji wa shilingi 387,630,957.04 kutekeleza mradi wa kupeleka majisafi katika Kata ya Uru Mashariki. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa chanzo kipya cha Mnini, Ukarabati wa tanki lenye ujazo wa $50m^3$ pamoja na upanuzi wa mtandao wa majisafi urefu wa kilometa 27. Kazi nyingine ni ukarabati wa tanki lenye ujazo wa $50m^3$ pamoja na ujenzi wa bomba la majisafi lenye urefu wa kilometa 15. Kazi hizi zimekamilika kwa kutumia mapato ya ndani ya *MUWASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali iendelee kutusaidia, kwani bado kuna uhitaji wa fedha kiasi cha shilingi 210,610,121.13 kwa ajili ya kukarabati mtandao wa bomba katika Vijiji vya Materuni, Mwasi Kusini na Kaskazini, Kyaseni, Mruwia na Kishumundu.

Mradi wa majisafi na salama katika Kata ya Old Moshi Mashariki, umegharimu shilingi 846,535,745.72. Kazi iliyofanyika ni uboreshaji na upanuzi wa mtandao wa majisafi kwa urefu wa kilometa 39.88 katika Vijiji vya Tsuduni, Kidia, Mahoma na Kikarara.

Mradi huu umetekelezwa na kukamilika kwa 100% kwa kutumia mapato ya ndani ya *MUWASA* na wananchi wameanza kunufaika na mradi kwa kupata majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaiomba Serikali itutengee fedha kwa ajili ya upanuzi wa mtandao wa bomba katika Vijiji vya Tsuduni, Kidia, Mahoma na Kikarara ili kupunguza gharama za maunganisho kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Uru Kusini yenye vijiji saba (Okaseni, Kimanganuni, Rua, Kariwa, Longuo A, Kitandu na Shinga) ina wakazi takribani 31,557 na ina miradi mitatu ya Mang'ana, Kisimeni na Mbora. Changamoto ya miradi hii ni maji kidogo katika mifumo ambayo hayatoshelezi. Naiomba Serikali isaidie, kwani mbali na hivyo vijiji kuna Taasisi ya Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge. Kuna shida kubwa sana ya maji hapo chuoni. Ninaiomba Wizara iangalie namna ya kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Arusha Chini yenye wakazi 13,977 kuna shida ya maji katika Vijiji vya Mikocheni na Chemchem. Sasa hivi ni watu wa Kirua Kahe wanatoa huduma ya maji ya kuuza katika maeneo haya. Maji huuzwa kwa bei ya juu na si salama kwa matumizi ya binadamu. Kata hii inahudumiwa na *RUWASA*. Ninaiomba Wizara ijenge mradi kwa kutumia maji ya kutoka Mto Ronga na Kikuletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Uru Kaskazini yenye wakazi 10,817 tunaiomba *MUWASA* iendelee kuwaunganisha wakazi wa Vijiji vya Msuni na Njari ili wananchi wapate maji.

Katika Kata ya Old Moshi Magharibi, kuna wakazi 8,431 na kuna mradi wa maji wa Tela Mande ambao umekamilika. Mradi huu una maji mengi sana na ya ziada ambayo kwa sasa yanahudumia wananchi wa ukanda wa milimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji na vitongoji vya kata hii vilivyopo ukanda wa tambarare kama kile cha Mandaka Mnono na Saningo havina maji ya bomba. Ninaiomba Wizara iwapelekee wananchi hawa walioko ukanda wa tambarare maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa uwekezaji wa shilingi 1,064,895,585.6 kwenye mradi wa majisafi katika Kata ya Kibosho Mashariki. Mradi huu utahusika na ukarabati wa chanzo cha Rumbanga ambapo utafanyika ujenzi wa chujio la maji *(treatment plant)* na upanuzi wa mtandao wa majisafi urefu wa kilometa 39.7. Tunaishukuru Serikali kwani mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka mfuko wa maji. Utekelezaji wa mradi huu umepangwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwani Kata ya Kibosho Kindi imepatiwa mradi wa majisafi wenye thamani ya shilingi 60,000,000 utakaohusu uchimbaji kisima kirefu cha maji *(borehole)*. Mradi huu utaanza kutekelezwa mwishoni mwa mwezi Mei, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba ni vyema Serikali iwekeze zaidi kwenye ulinzi wa vyanzo vyote vya maji hapa nchini ili kulinda haki ya kimsingi ya wananchi kupata maji safi na salama ya kunywa, wakiwemo wale wa Jimbo la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kubwa kwa niaba ya wananchi wa Iringa Mjini, tunaomba tutoe shukrani zetu za dhati kwa huduma bora kabisa ya maji katika mji wetu wa Iringa. Upatikanaji wa maji Iringa Mjini ni karibu 98%. Huduma ya kutatua changamoto na matatizo ya wananchi yanafanyika kwa ustadi, utu na upendo mkubwa na kwa njia za kisasa kabisa za kidijitali. Mheshimiwa Waziri naomba sasa kwa ajili ya Iringa Mjini, kama unavyojua maeneo mengi ya mjini huduma za jamii kama shule na vituo vya afya, zahanati na hospitali zinatumika na watu wengi hata wa kutoka maeneo mengine ya majimbo ya vijijini. Shule zetu nyingi za kata ni za hosteli na ni kwa watoto wa kike. Maji ya bomba ni changamoto. Ninaomba muone kwa ngazi ya Wizara msaidie hizi baadhi ya shule za mjini zichimbiwe visima hasa zenye uwezekano

wa kupata maji. Pili eneo la Ugele na Mosi tuchimbiwe visima virefu. Ahsante na nashukuru.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake kwa Taifa letu nyanja mbalimbali za ustawi wa kijamii kisiasa, kiuchumi, kidplomasia, amani na mshikamano, ahsante sana muumba wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa jimbo langu la Mbulu Mjini kushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi alivyotekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi yam waka 2020/2025 Mwenyezi Mungu awabariki sana, sisi wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini tutamlipa fadhila zake katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2025 kwa kumpigia kura nyingi za imani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jumaa Aweso - Waziri wa Wizara hii muhimu sana, nampongeza sana Mheshimiwa Andrew Kundo - Naibu Waziri, Katibu Mkuu *Engineer* Mwajuma Waziri, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wakuu wa Wizara hii kwa ujumla wao na naipongeza pia hotuba nzuri sana ya Mheshimiwa Waziri aliyoiwasilisha mbele ya Bunge letu hivi punde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuipongeza sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa taarifa yao waliyoiwasilisha mbele ya Bunge letu kwa kweli imefafanua hali halisi na changamoto mbalimbali na mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo hayo bajeti ya Wizara hii muhimu sana; kwa kuwa tumefanikiwa sana kuchimba visima vingi sana kupitia *RUWASA* katika majimbo mbalimbali nchini hali iliyowapa matumaini makubwa wananchi wetu kupata huduma bora ya maji safi na salama maeneo mengi. Hivyo basi tunaiomba Serikali

yetu ijitahidi kupeleka fedha zinazoombwa kwenye bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Mbulu Mjini naishukuru sana Serikali yetu kwa kubuni mradi mkubwa wa maji wa Mto Tsoray katika tarafa nzima ya Nambis ambao utasaidia kutatuta tatizo la maji katika vijiji zaidi 28 katika Halmashauri ya Mbulu Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ninaiomba sana Wizara kuharakisha utekelezaji wa mradi huu kwa kuwa wananchi wangu wanausubiri kwa haiba kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa mpango wake wa kuchimba visima 900 nchini ambapo kila jimbo limefanikiwa kupata visima vitano. Hivyo basi tunaiomba Serikali yetu itafute fedha za kujenga miundombinu ya kusambaza maji kwenda kwa wananchi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja 100% na naomba kuwasilisha.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya katika sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nikupongeze wewe kwa kazi unayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi; naomba mradi wa Ziwa Victoria kuja Urambo ukamilike na pia naomba Bwawa la Karemera likamilike.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Newala Vijijini lina changamoto kubwa sana ya maji kiasi kwamba kila nyumba inayojengwa mwenye nyumba hujenga kisima chake cha kuvuna maji yasiyo salama sana kwa kuwa visima vingi huokota maji yanayotiririka ardhini na hayatibiwi kabisa kiasi kwamba inahatarisha afya za wananchi, lakini pia

maji ni muhimu sana kwenye kilimo kwa kuwa upuliziaji wa viuatilifu vya maji/sumu hutumia maji. Naomba kushauri kwamba Serikali ikubali kujenga malambo ya kukusanyia maji yaweze kutumika kwa matumizi ya majumbani, kwenye kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali kwenye mwaka wa fedha wa 2024/2025 ilishapeleka fedha kiasi cha shilingi 1,035,972,511.12 kwenye Jimbo la Newala Vijijini, tunaomba matokeo ya uwekezaji huo yaonekane kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya mkandarasi wa Mradi wa Miji 28; tunaiomba Serikali imlipe kiasi cha shilingi bilioni tatu alizoomba mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji wa Miji 28 wa Makonde. Mradi huu ndio mkombozi mkubwa wa wananchi wa Newala ambao wanapata shida ya maji kwa muda mrefu ukizingatia kuwa maeneo ya kupata maji kwa urahisi katika Wilaya ya Newala ni shida kutokana na mazingira ya kijiografia yaliyopo Newala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tufanye jitihada za makusudi ili kuwanusuru wananchi ukizingatia kuwa hali ya hewa mwaka huu haikuwa rafiki sana kwa kuwa mvua sio nyingi na visima vingi vya wenyeji havina maji ya kutosha hali ambayo inaweza kusababisha changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utunzaji wa vifaa/mabomba ya maji; wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji ya Mnima - Miyuyu wameacha mabomba barabarani kwa muda mrefu hasa katika Kata ya Mikumbi hali inayosababisha mabomba hayo kuungua moto, kukatwa na wananchi pamoja na kukanyagwa na magari. Hii inasababisha hasira kwa wananchi wanaosubiri huduma ya maji, lakini pia inarudisha nyuma jitihada za Serikali za kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi kwa haraka. Nashauri usimamizi wa karibu wa wakandarasi hawa ukizingatia kuwa mradi huu ni wa muda mrefu tangu mwaka 2018 na ulikuwa mradi wa miezi tisa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bili za maji; nashauri matumizi ya *prepaid* mita ili kuondoa changamoto ya malalamiko ya bili kwa wananchi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Rais mpendwa Mama yetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuletea miradi mingi katika Jimbo la Lushoto ikiwemo miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lushoto lipo milimani na kwa bahati nzuri Mungu ametujaalia vyanzo vingi vya maji. Tunachohitaji kwa sasa ni miundombinu ya maji kama vile matenki pamoja na mabomba kwa ajili ya kusafirisha maji hayo ya mserereko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna chanzo chetu cha maji ambacho kina uwezo wa kusambaza maji kwenye jimbo lote la Lushoto isipokuwa kata mbili tu ambazo ni Kata ya Kilole na Ngwelo kati ya kata 15 za Jimbo la Lushoto na mradi huu ukitekelezeka na ukakamilika una uwezo wa kupeleka maji katika Wilaya ya Korogwe na Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ulishatembelewa na Mkurugenzi wa *RUWASA* na alishuhudia kuwa chanzo kile ni cha uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba mradi huu utengewe fedha kwenye bajeti hii ili wananchi wa Lushoto waondokane kabisa na kero ya maji na kwa bahati nzuri mradi huu umeshatengewa pesa za upembuzi yakinifu, ila sijajua mpaka sasa upembuzi huu uliishia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, pamoja na kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji Ndugu Jumaa Aweso pamoja na timu yake yote kwa kazi kubwa wanayoifanya.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza na kumshukuru mpendwa Rais wetu, Dkt. Samia

Suluhu Hassan, kwa fedha nyingi alizoidhinisha ziwekezwe kwenye miradi ya maji Vunjo takribani shilingi bilioni 12 ndani ya miaka minne. Ninapongeza pia Waziri wa Maji, Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na timu yake Naima Waziri, Mkurugenzi Mtendaji wa *RUWASA* na Mamlaka za Maji Mkoani Kilimanjaro kwa kusimamia vyema matumizi ya fedha hizi na miradi yenye thamani ikapatikana na hivyo kumtua mama ndoo kichwani kwa kiwango kikubwa kwenye Jimbo la Vunjo. Hata hivyo ninamuomba Mheshimiwa Waziri atoe fedha ili miradi inayoendelea kutekelezwa kwenye Kata za Mwika Kusini, Mwika Kaskazini, Marangu Magharibi na Marangu Mashariki ikamilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri utaratibu wa sasa wa kukatisha huduma ya maji mashuleni na kwenye vituo vya afya mara tu wanapochelewesha kulipia huduma hii iangaliwe upya.

*Hapa Naibu Spika (Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa kutokana na…., Mheshimiwa Naibu Waziri jibu kwa dakika tatu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii nami niweze kuongea mawili, matatu, lakini kikubwa sana Waheshimiwa Wabunge wameongea, Bunge limeongea maana yake Watanzania wameongea na kikubwa zaidi wamepongeza kazi kubwa sana ambayo imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan leo nasimama hapa nikiwa katika bajeti ya tano nikiwa Naibu Waziri, imani hiyo namshukuru sana kwa kunipatia na hiyo ni heshima kwa wananchi wa Jimbo la Bariadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana kaka yangu Jumaa Hamidu Aweso. Kaka yangu huyu…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante. Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nikushukuru wewe binafsi, lakini niwashukuru Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango yenu na ushauri wenu ambao na pongezi zenu ambazo mmezitoa katika Wizara yetu ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna maneno matamu sana ya kusema zaidi ya kusema ahsanteni sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ambalo ninataka kusema Waheshimiwa Wabunge mmechangia katika bajeti yetu ya Wizara ya Maji, niwaahidi kila Mbunge ambaye amechangia katika bajeti yetu ya Wizara ya Maji tutawajibu kwa maandishi ili kuhakikisha kwamba tunaleta kumbukumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa nitumie nafasi hii nami niungane na Waheshimiwa Wabunge kwa dhati ya moyo kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hakuna hata mmoja ambaye asiyejua. Mimi nimepata bahati ya kuwa Mbunge katika kipindi cha miaka kumi sasa na mimi ni Mbunge hakuna sekta ambayo ilikuwa ya kero na lawama kama Wizara Maji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri toa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kusema dhati tu ya moyo, Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiyo suluhu ya matatizo ya Watanzania hasa katika kumtua mwana mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naomba kutoa hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imepokelewa

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*......................................Sh.3,761,486,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sijapata mpaka sasa hivi majina ya mshahara wa Waziri. Tunaingia kwenye *guillotine*.

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*...............Sh.1,344,944,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*....................Sh. 2,252,210,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*.....Sh. 535,277,000
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*................................Sh. 566,441,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 821,547,000
Kifungu 1007 - *Management Information System Unit*.............................................Sh. 547,123,000
Kifungu 1008 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 718,259,000
Kifungu 1009 - *Project Preparation, Cordination & Environmental Management Unit*........Sh.755,420,000
Kifungu 1011 - *Monitoring and Evaluation Unit*...........Sh. 601,176,870
Kifungu 2001 - *Water Resources*.............................. Sh.12,159,143,093
Kifungu 2003 - *Water Laboratory*..............................Sh. 4,086,961,000
Kifungu 3001 - *Water Supply and Sanitation Division*..............................................Sh.40,281,683,359
Kifungu 5001 - *Water Development & Management Institute*................................................Sh. 5,347,907,678

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*..........................................Sh. 801,700,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.................Sh.180,805,697,000
Kifungu 2001 - *Water Resources*...............................Sh.12,542,460,000
Kifungu 2003 - *Water Laboratory*...............................Sh. 1,713,105,000
Kifungu 3001 - *Water Supply and Sanitation Division*............................Sh.144,600,694,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2025/2026 – Wizara ya Maji Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hongera sana, umefanya kazi vizuri sana, umepokea maelekezo ya Mheshimiwa Rais vizuri sana, nakumbuka tulivyokuwa Same Mheshimiwa Rais alikupigia saluti wewe na timu yako. Hongereni sana kwa kweli mnajitahidi na mmeleta mabadiliko makubwa niombe tu mjaribu kutazama maeneo ya mjini mjini Dar es Salaam pale bado kuna shida hapa na pale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo asubuhi hii; wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Waziri wa Maji kutoa Mkoa wa Tanga wakiongozwa na Ndugu Mohamed Faki, Katibu Tawala Wilaya ya Muheza na Ndugu Salum Palango, Katibu Tawala Wilaya ya Mkinga. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Edger Mtitu, Diwani wa Kata ya Lobonde kutoka Wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo; Wanafunzi 90 na walimu wao nane wa Shule ya Awali na Msingi ya Fountain Gate ya Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 27 na walimu saba wa Shule ya Awali na Msingi Theresiani ya Jijini Dar es Salaam, hongereni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana, sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 05:43 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 12 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*